# *Zeri Katika Gileadi*

. . .sema mengi. Hebu tuendelee tu kusimama kwa muda kidogo kwa ajili ya maombi. Daima ninapenda kuzungumza na Mwandishi kabla sijafungua Kitabu Chake. Hivi hamwoni hilo ni wazo zuri?

2 Mtu fulani alikuwa akizungumza wakati mmoja, nikasema *kitu fulani*, ndipo—ndipo mtu huyo akasema, alikuwa ni rafiki yangu mwema, karibu ninyi nyote mnamfahamu, naye anahubiri katika lugha saba, Booth-Clibborn, mmesikia habari zake, nadhani, William Booth-Clibborn, naye akaniambia, akasema, "Lakini, Ndugu Branham, huijui tu Biblia yako."

3 Nikasema, "Lakini ninamjua Mwandishi wake vizuri sana." Hiyo ni. . .?. . .Kama ninamjua Mwandishi, basi nafikiri ya kwamba Yeye atanifundisha Neno Lake. Kwa hiyo, hebu na tuzungumze Naye sasa, kabla hatujaingia katika Neno Lake.

4 Baba yetu wa Mbinguni, Mwandishi wa Neno hili, Mwandishi wa Neno la Mungu, "Neno alikuwa Mungu na akafanyika mwili, akakaa kwetu," tunakujia Wewe katika Jina la Yesu, Mwanao, Mwokozi wetu. Tunampenda, Baba, kwa sababu kwamba Yeye alikuwa mtiifu hata kufa. Ile ghadhabu iliyopaswa kuja juu yetu ilimwagwa juu Yake pale Kalvari, hapo aliteseka badala yetu ili tuwe huru. Si ajabu watu kamwe hawajaweza kuelezea upendo aliokuwa nao Baba kwa jamii iliyoanguka ya Adamu, kumtoa Mwanawe apate kuteswa, apate kutukomboa kwa neema Yake.

5 Na, Baba, tunaomba, usiku wa leo, ya kwamba utatubariki katika jitihada zetu, usiku wa leo, tunapokuja kwenye ushirika wa Neno. Neno na liwe taa ya miguu yetu, Nuru itakayotuongoza, vilindi zaidi, na vimo vya juu zaidi katika upendo wa Mungu. Pia uwaponye wagonjwa usiku wa leo, Baba. Huu ndio usiku ambao tunapaswa kuwaombea wagonjwa, tunaomba ya kwamba utamponya kila mmoja wao.

6 Bariki kanisa hili dogo, Ee Mungu, mbariki maskini mchungaji wake wa thamani, Ndugu Buntain, na ndugu yake mpendwa ambaye ndiyo kwanza nikutane naye na kupeana mikono naye kutoka Calcutta, ninaomba, Baba, ya kwamba utawabariki wavulana hawa. Basi wazia juu ya baba yao mzee mcha Mungu huko juu, na wakati alipowabeba kote kama wavulana wadogo, jinsi, labda, aliamini ya kwamba Wewe siku moja ungewafanya wahudumu namna hii, nasi tuna furaha, Bwana, Mungu hujibu maombi, tunajua hilo. Kwa hiyo, jibu yetu usiku wa leo, Baba, na upate utukufu kutokana na kukusanyika kwetu pamoja. Tunaomba, katika Jina la Yesu. Amina.

7 Mwaweza kuketi. Haya ni majaliwa makuu sana kukusanyika katika ibada ya Mungu. Nanyi mwajua, wakati umewadia wa kuondoa hisia zote za kigeni, ndipo wakati wa kuondoka umewadia, mnaona. Tunapoingia, na sikuzote tu katika kusema, "U hali gani?" halafu huduma yote ni mpya, nami ni mpya na jambo la kwanza mwajua inachukua muda kidogo kwetu sote kufahamiana, kumwacha Roho Mtakatifu atende kazi miongoni mwetu tupate kuona ya kwamba sisi ni ndugu na dada, mnaona, kwamba hatuna shida yoyote, nasi ni watoto wa Mungu tu.

8 Na huduma ambayo Mungu alinipa, mbona, ni kwa ajili yenu, na ni upendo, madhihirisho ya upendo. Halafu basi tunasema, "Kwaheri," kisha tunaondoka kwenda mahali pengine. Nami nilijaribu, siwezi kukumbuka jina hilo la mahali hapo, ninapaita . . . Billy alisema, "Unafikiri tunaenda wapi, Baba?"

9 Nikasema, "Venezuela." Huko kungekuwa ni mbali sana, sivyo? Lakini hata hivyo, tumekuwa Venezuela, tumekuwako, kamwe hatukuwa na ibada kule.

10 Lakini—lakini tunatarajia Bwana akipenda . . . Nilikutana na rafiki yangu mwema Ndugu Kopp kule nyuma, naye anataka, atualike California tena, na—na halafu sehemu mbalimbali kote katika mataifa. Nasi hatuna budi kumalizia mahojiano yetu yote ambayo—ambayo . . . Jinsi tunavyofanya jambo hilo . . . Mchungaji alikuwa akisema jambo fulani hivi majuzi, jinsi hayo mahojiano tuliyozungumzia.

11 Vema, kuna—kuna mambo katika maisha ya watu ambayo hawajui waelekee wapi, wako tu—wako tu mwishoni mwa safari, hivyo tu. Hawajui . . . Ninaamini ya kwamba Neno la Mungu hutatua kila kitu tunachohitaji, hivi hamwamini hivyo? Hiyo ni kweli. Lakini sasa, kwa mfano, kama lingesema jambo fulani kuhusu wokovu, basi Neno la Mungu linaelezea hilo.

12 Sasa, lakini vipi kama ni jambo ambalo Neno la Mungu halijaandika *Hapa*? Basi Mungu hahitaji chochote, Yeye hutuma karama mbalimbali kushughulikia hilo. Halafu basi, katika Agano la Kale sisi . . . Bwana alitupa watu ambao wangewaendea, na kuwataka shauri na kuwauliza kuhusu yatakayotukia. Nao walilelewa tangu utotoni na kuendelea, nao walikuwa na Neno la Bwana, nao wakajisikia wamehakikishiwa kwamba kama mwonaji huyu angeweza kuona yale Bwana aliyowaambia, vema, hilo—hilo—hilo lilitosha.

13 Vema, mimi si mwonaji, mimi si nabii, bali mimi—mimi ni maskini Mmataifa ambaye Bwana ananiruhusu nitumiwe kuwasaidia watu wa Mataifa katika siku hizi, mnaona. Ninaamini imechukuliwa mahali fulani katika Biblia kama namna fulani ya karama, lakini hata iweje, hiyo, ni ndogo, na

huo sio umuhimu wake, ni kile tunachoweza kufanya kumsaidia mtu fulani kumkaribia Mungu zaidi.

14 Na jinsi tunavyofanya, watu huandika nyumbani, kisha tunapata anwani zao, kisha tunaandika jina, halafu tunawatumia kadi tena. Na mahali popote katika jamii hiyo, katika jamii hiyo, halafu tunawatumia habari ni nani atakayekuja. Vema, basi wakati wa mchana, kama hapa sababu ya wengi wenu kutojua ni kwa nini hatukuwa na ibada hizi za upambanuzi kila usiku, mbona, mchana huondoa zote, mnaona, nawe ni dhaifu sana na umechoka, hata huwezi kufanya hivyo usiku.

15 Na kwa hiyo sisi. . .Watu huingia na kuketi chini. Sijui hao ni akina nani, siwaulizi. Nasi tunangojea tu pale mpaka Roho Mtakatifu atakapokuja na kuanika kitu hicho chote, anawaambia yale wamefanya, ambapo walifanya kosa lao, yale wanayopaswa kufanya, na—na kila kitu jinsi tu. . .

16 Nanyi mngeshangaa, madaktari, wanasheria, wafanyabiashara, na kadhalika kutoka kote nchini, kutoka Afrika, kutoka Asia, kutoka Ujerumani, kutoka Uswisi, wanatoka kote nchini, wameketi mle ndani wakingojea, miezi, na kadhalika. Nasi tunawaandikia tu, badala ya hao wote kulundikana kule, kisha wengi wao wanarudi nyumbani wamevunjika moyo, tunangojea tu mpaka wakati wao utakapofika ndipo tunawaingiza.

17 Sasa, California, hapa, tuna mikutano. Na hapa baadhi ya watu wamekuwa wakingojea yapata miaka mitatu au zaidi. Halafu basi, mara tunapoweza kuwafikia, hatuondoki, tunakaa papo hapo mpaka Roho Mtakatifu atakaponena. Ndipo wanajua la kufanya, anawaambia jinsi ya kulifanya, na jinsi lilivyo, na kamwe halijawahi kushindwa hata wakati mmoja, kwa sababu ni Mungu. Tunashukuru kwa ajili ya jambo hilo, tunamshukuru sana Baba yetu wa Mbinguni ambaye. . .na wahudumu kwa mamia. Kwa hiyo tu—tuna chumba tunachowapeleka, nao wanajua wakati wa miadi yao, na ni lini hasa. Ndipo ni. . . tunakuja tu. . .

18 Sasa, wakati mwingine nitakuwa nje nikitembea huku na huku, ama labda katika maombi kwa ajili ya mtu mwingine, Naye atanionyesha ono la mahali nitakapoenda kukutana na mtu fulani, ama kufanya jambo fulani, ndipo ninaondoka moja kwa moja na kufanya hivyo sasa hivi, kwa sababu huyo ni Mungu Mwenyewe anayenena, akiitumia, mnaona. Kwa hiyo sikuzote mimi hufanya tu vile. . .hujaribu kufanya anavyoniambia. Nasikitika kusema ninamkosea mara nyingi sana. Ninajionea aibu mbele ya Kanisa Lake usiku wa leo, kufanya maungamo kama haya, lakini kuna mara nyingi ambapo—ambapo nimemkosea, nami. . .Niombeeni ya kwamba

mimi—ya kwamba sitampungukia zaidi ya iwezekanavyo kibinadamu.

19 Mimi, mara nyingi, najua kama ningalienda na kufanya mambo fulani, ingekuwa tofauti. Lakini mtu fulani tu akikuvuta *huku*, na mtu fulani akivuta *huku*, na—na ni—ni vigumu sana, na ni marafiki wazuri unaowapenda sana, na—na wakati mwingine unatoka nje ya mapenzi ya Bwana, hata hivyo, kwa namna fulani ni huduma mbili. Hii ni huduma ya kiinjilisti. Hiyo nyingine . . . Mnakumbuka jinsi wale waonaji wa kale walivyofanya? Walikaa huko nje nyikani, wakakaa huko nje mpaka Mungu alipowaambia wafanye jambo fulani, wanaingia moja kwa moja kwa kishindo, wanatoa ujumbe wao, kisha wakarudi nyikani tena. Mnaona? Na hiyo ndiyo tofauti yake.

20 Sasa, lakini tuna furaha sana kujua ya kwamba Baba yetu wa Mbinguni, wa Agano la Kale, Yule yule aliyekuwa ndani ya Yesu Kristo Mwanawe, ndiye Yule yule katika Kanisa Lake leo, mnaona. Loo, hilo si linauchangamsha tu moyo wako kujua ya kwamba katika siku ambayo kuna mengi sana . . .? Wanasema vema, madhehebu mbalimbali yanasema, "*Tunayo*, njoo huku." Mataifa mbalimbali yanasema, "*Tunayo*, njoo huku." Lakini Yeye Ndiye aliye *nayo*.

21 Kwa hiyo, tuna furaha sana kwamba Yeye hushuka na kututhibitishia kwa Biblia, yale tu atakayofanya, na kushuka na kufanya yale hasa aliyosema angefanya, ndipo tunaangalia huko nyuma katika Biblia na kuona tu ukurasa kwa ukurasa ukifunuliwa kama vile Yeye alivyosema angefanya. Ajabu, ajabu!

22 Ni wangapi walio na Sauti ya Wafanyabiashara wakati huu? Sauti ya Wafanyabiashara. Ninathamini makala hiyo ndogo, ono hilo, aliweka sehemu yake mle ndani ambayo ni nzuri sana ambayo, nadhani iliandikwa na Ndugu Tommy Hicks. Hilo—hilo lilifanya badiliko ndani yangu. Sikuzote niliogopa kifo, nilifikiri ningeninii . . . sikutaka kuwa roho.

23 Kamwe si—sikujua chochote, hiyo ndiyo sababu Malaika wa Bwana, Yule ambaye hunena nami, ninajua ni wa Mungu. Kwa sababu Yeye . . . Kwanza, kama angeniambia jambo moja ambalo halikuwa ni Neno la Mungu, nisingeliamini. La, bwana. Sijali ni nini, halina budi kuwa ni Neno la Mungu. Mnaona? Na kuna malaika wa kila namna mwajua, tunajua hilo. Lakini ninii . . . Paulo alisema, "Kama Malaika akija na kuhubiri injili nyingine yoyote isipokuwa hii niliyoihubiri . . . " Mnaona?

24 Basi nilipofika kule, na maskini hii, sijui, sitaki kusema, kumwiga Mtakatifu Paulo mashuhuri, la hasha, nisingefanya hivyo kwa chochote, sijui, labda lilikuwa ni ono, lakini kuna jambo moja nijualo, sikuwa nimelala. Na—na kama lilikuwa ni ono, sijawahi kuwa na moja kama hilo hapo awali maishani mwangu. Nilikuwa tu juu kama hizo nguzo chomozi, ama viguzo

chomozi, mnavyoviita *kule*, vile vigae vya dari *pale*, nilikuwa tu juu hivi nikijiangalia mwenyewe. Na kadiri tu ninavyosimama papa hapa, nikiangalia moja kwa moja nyuma, na ningeweza kujiona nimelala pale, nilikuwa na hisi ya ajabu sana, nilifikiri nilikuwa na mshtuko wa moyo na nilikuwa nimekufa. Ndipo nikawazia, "Vema, kama hii ni mauti, jamani, hii ni nzuri sana!"

25 Nami na—nawaambia ninyi Wakristo sasa hivi, hamna hata jambo moja la kuwatia wasiwasi, endapo mko ndani ya Kristo. Kamwe msiogope mauti, kifo hakina hofu, la, la, la, ni furaha.

26 Nami nilikutana na hao wanawake kule. Na, kwa kweli, ni—ninahisi, wakati mwingine, nimekuwa mkali kidogo kwa dada zangu. Mimi. . .Sio—sio kujaribu kuwa katili, bali si—siwataki wawe kama walimwengu wengine, nina—ninawaonea wivu. Mnaona? Mimi, ninii tu, ni—ninataka wawe Wakristo halisi, ninataka waonekane hivyo, watende hivyo, na wawe hivyo, na wawe halisi.

27 Mimi, na hiyo ndiyo sababu nina bidii kwa ajili ya ndugu zangu. Siwataki waende kombo katika maskini injili za kijamii, kama mnavyopata kwenye kiangulio fulani hapa nje, ninawataka wawe watu halisi wa Mungu, wasimame wala wasipatane juu ya Neno hilo, kweli waliweke huko nje. Hiyo ni—hiyo ni. . .Si kwamba ninajaribu kuwaudhi ndugu zangu, na—nawapenda sana siwezi kufanya jambo hilo, ninawapenda watu sana siwezi kufanya hivyo. Lakini, kwa kweli, upendo hukata, mlijua hilo?

28 Sasa, mama, ninataka kukuuliza jambo fulani, ama binti ambaye bado si mama bado: Kama—kama mama yako, ama mtoto wako, alikuwa hapa nje mtaani, nanyi mnawajua maskini hao wahaini wanaopitia kwenye barabara hiyo, nao wamelewa nusu, na kila kitu, mtoto huyo atauawa, wala asingekaa nje ya barabara, ungesema, "Vema, kipenzi, endelea tu ukaketi barabarani, nadhani hilo litakuwa sawa"?

29 Si ninii. . .Usingempenda mtoto huyo mchanga kama ungetenda namna hiyo. Upendo halisi ungetoka huko nje, nawe ungemweka chini ya nidhamu kali na kumcharaza, mpaka aondoke barabarani. Hiyo ni kweli? Basi msinikasirikie. Mnaona? Nawatakeni tu mkae mbali na mambo ya ulimwengu, hivyo tu, kaeni tu mbali nayo, myaondokee.

30 Sasa, madhehebu, mnanisikia nikiyashambulia mara moja moja. Sasa, sikusudii kusema madhehebu hayako sawa. La, bwana. Lakini mnaona, unafikia tu mahali unaposema, "Mimi ni mfuasi wa Church of God." "Mimi ni mfuasi wa Assemblies." Hiyo ni kama tu vile mlivyozoea kumdhihaki Mmethodisti akisema hivyo, na Mbaptisti na Mpresbiteri, nasi tukaingia moja kwa moja katika uozo ule ule. Mnaona? Sasa, hayo ni sawa, Methodisti ni sawa, Baptisti ni sawa, Assemblies of God, Church of God, hao wote, ni sawa.

31 Lakini ndugu, wakati, mnaona, haidhuru ni wapi, sasa, watu wenye nia ya kiroho, natumaini mnaelewa, mtaangalia, kwamba muda si muda mwajua, kama tu ile awamu ya kwanza ya mitume, wote walijazwa Roho, awamu ya pili ikaanza kupotoka, ya tatu ikapotoka tena, na katika awamu ya nne, wakaingia moja kwa moja katika upagani. Ndipo basi Urumi, na Upagani, na Ukristo, na kadhalika wakaunganika pamoja na kufanya kanisa la ulimwengu mzima. Na kutoka hapo . . .

32 Mnaona, hilo ni jambo lile lile, Martin Luther alikuwa na uamsho halisi, wakati Luther alipokuwa hai, aliuweka sawa. Je, mlijua Martin Luther alinena kwa lugha? Naam, bwana, hakika alinena. Naye alikuwa na ishara kuu na maajabu. Lakini wakati Luther alipokufa, ni kitu gani kilichotukia? Kanisa liliunda madhehebu, na hapo likapotea. Awamu nyingine ilikuwa imetokea kupitia kiangulio, nao wote hao wakaondoka.

33 Sasa, mnaona, Martin Luther, ilitokea kwamba aliiona ile Nguzo kuu ya Moto, naye akaifuata. Na, lakini alifanya nini . . . walifanya nini? Waliunda madhehebu papa hapa chini ya Nguzo hii ya Moto, wala huwezi kumwundia Mungu dhehebu. Kwa hiyo, ile Nguzo ya Moto ikasogea, naye Luther asingeweza kuifuata kwa sababu alikuwa ameunda dhehebu.

34 Ndipo John Wesley akaiona, naye akaenda kwenye utakaso. Nao walifanya nini baada ya siku za Wesley? Waliiundia dhehebu. Nayo ilifanya nini wakati ubatizo, ndipo ikaondoka tena, ubatizo wa Roho Mtakatifu? Ndipo Wapentekoste wakaiona, nao hao wakaifuatilia. Lakini walifanya nini? Jambo lile lile hao wengine walilofanya, wakaunda madhehebu papo hapo chini yake. Baada ya awamu ya kwanza ya wale baba wazee, yapata miaka arobaini, hamsini iliyopita, jamaa hawa vijana waliingia, ndipo hao vijana na wajukuu wakaanza kuja. Haya basi, mnaona, moja kwa moja nyuma, jambo lile lile.

35 Lakini kumbukeni, ndugu, Ujumbe huo unapaswa kulitikisa taifa, ama, kulitikisa Kanisa. Msiangalie ati *kitu fulani* kikuu kishuke kwenye ushoroba wote, Ujumbe wa Mungu utakuwa hasa kwa Kanisa teule. Ishara hizi na maajabu kamwe hayatafanywa mbele ya ulimwengu, hayapaswi kufanywa.

36 Rais wa Four Rose Whiskey Company, mke wake alikuwa, yeye ni wa Muungano wa Kimishenari, naye alikuwa katika mmoja wa hiyo mikutano, akampigia simu Ndugu Bosworth, ambaye alikuwa ni wa Muungano wa Kimishenari, naye kasema, "Jambo ni kwamba, huachi karama hiyo ianze kupanuka." Kasema, "Yale niliyoona jana usiku yangelifanywa katika miji mikuu, na kadhalika, ya taifa, mbona," kasema, "yangeongoa, yangeuleta ulimwengu mzima kwenye Ukristo." Lakini mnaona, hayapelekwi kwenye miji mikuu ya mataifa, mnaona, yanapelekwa kwa Kanisa teule. Mnaona, wewe si . . .

37 “Loo,” wao wanasema, “andika jina lako kwenye vibao vikubwa mno, halafu uingie kwenye vituo vikubwa, ingia kwenye televisheni.” Haikukusudiwa hiyo, nilitumwa tu kwenu, Kanisa, mnaona, hilo ndilo. Sasa, wewe liamini kwa moyo wako wote.

38 Ninataka kusema hapa, wakati nikiwa kanisani, huu bila shaka umekuwa ni wakati mzuri sana kwetu, tunamthamini Ndugu Buntain, na kwa wafanyakazi wenza, na ndugu, ninyi watu wote. Na hasa sana ninyi watu, wakati ibada zisizo za uponyaji, mkija tu na kusimama hapa, nikiendelea kulima, na kuliacha tu lianguke popote litakapo, na, bali nikidumu tu mwaminifu kwa Neno.

39 Sijasema neno moja ambalo ningelighairi, wala sijasema neno moja ambalo Biblia haisemi, hiyo ni kweli, ama ninaweza kulithibitisha kwa Maandiko, kwa hiyo limekuwa sawa na Neno. Naye Roho Mtakatifu mbarikiwa amekuja moja kwa moja wakati wote, akilithibitisha Neno moja kwa moja, vivyo hivyo hasa.

40 Nanyi watu wapendwa mmekuja kila usiku, na kupajaza mahali hapa, na kuja moja kwa moja. Ninathamini hilo, hilo ni zuri kweli. Ninaomba ya kwamba hakuna hata mmoja wenu atakayepotea, kila mmoja wenu angekuwa katika Ufalme wa Mungu, na, ninaomba.

41 Ninaomba ya kwamba kutakuwa na . . . uamsho huu kamwe hautaisha katika kanisa hili dogo la Assembly of God hapa pembeni. Ninaomba ya kwamba Nuru na nguvu za Mungu zitaenea kutoka hapa, mpaka ishike Pwani yote ya Magharibi, nami na—natumaini ya kwamba hili litakuwa ni kanisa la mfano, ninaamini. Na Assemblies of God wengine, na Wabaptisti, na Wamethodisti, na kila mahali, na kushika tu moto, kila mahali.

42 Mnaona, ndugu, hatujagawanyika, ha—hatuwezi kugawanyika, sisi ni wanadamu. Mwajua, Wamethodisti hula chakula cha namna ile ile mnachokula? Wabaptisti hufanya vile vile. Wakatoliki wanawapenda watoto wao kama tu vile mnavyowapenda wenu; wanaume Wakatoliki wanawapenda wake zao kama mnavyowapenda wake zenu, na waume, wake wanapendana; wanataka kwenda Mbinguni kama vile ninyi mnavyotaka kwenda. Mnaona?

43 Kwa hiyo tofauti zetu ndogondogo, hebu tusahau hizo, hebu tumkumbatie kila mtu, tuwaendee tu, na kuwavuta ndani, katika upendo kwa Ufalme wa Mungu.

44 Mnaona kile Yeye alichoniambia? Daima nimeamini, na daima ninaamini, ya kwamba nguvu hizo za upendo zimezidi kunena kwa lugha, zimezidi kupiga kelele, zimezidi kila kitu nijuacho, daima zimekuwa ndizo wimbo wangu:

> Mpendwa Mwana-Kondoo anayekufa, Damu
> Yako ya thamani

Kamwe haitapoteza nguvu zake,
Mpaka Kanisa lote la Mungu lililokombolewa,
Litakapookolewa lisitende dhambi tena.

Tangu kwa imani nilipokiona kile Kijito,
Kinacholetwa na majeraha yako,
Upendo wa ukombozi umekuwa ndio wimbo wangu,
Na utakuwa hivyo hata nitakapokufa.

45 Basi kama kweli ninalipenda Kanisa la Mungu, ambalo Kristo alinunua kwa Damu Yake Mwenyewe, ninawezaje kutulia na kuliona likizidi kuwa mbaya? Siwezi kufanya hivyo, siwezi kabisa, ndugu. Kama ndugu zangu wakinifukuza, si—siwezi kujizuia, mnaona, lakini si—sina budi kudumu mwaminifu kwa Neno hili, mnaona, ni—ni kazi yangu.

46 Sasa, tutakuwa na mstari wa maombi usiku wa leo, na kuwaombea wagonjwa. Na kwa hiyo, nina hakika ya kwamba hiyo ingekuwa ndiyo njia nzuri ya kufunga ibada hapa kanisani. Nao wananiambia ya kwamba walinipa sadaka ya upendo hapa kanisani. Vema sasa, si—sikuomba hilo, enyi marafiki, sikuja hapa kwa ajili ya jambo hilo, nilikuja kwa ajili ya ushirika pamoja nanyi, na pamoja na maskini mchungaji wenu hapa, mimi, hilo ndilo lililonileta hapa, si sadaka. Kama kamwe hamkutoa senti moja nyekundu, mngeninii. . .Ningekuwa tu vile vile, mnaona, Ni—ninalithamini vivyo hivyo, mnaona, na si mahali. . .

47 Sijawahi kamwe maishani mwangu, nina umri wa miaka hamsini na mmoja, nimekuwa nikihubiri Injili kwa miaka thelathini na mmoja, niliichunga Maskani ya Kibaptisti kwa muda wa miaka kumi na saba, wala kamwe sikuchukua sadaka maishani mwangu, kamwe maishani mwangu. Nilifanya uchungaji miaka kumi na saba katika kanisa la Kibaptisti kule Jeffersonville, Indiana, wala kamwe hata sikuwa na sahani ya sadaka kanisani. Hiyo ni kweli. Si kwa sababu hawangefanya hivyo, ni kwa sababu niliweza kufanya kazi, kwa hiyo nilitoka tu na kufanya kazi, kazi ngumu, pia, kutembea maili thelathini, thelathini na tano kwa siku, nikifanya doria, na mambo kama hayo, kupitia nyikani, na kufanya kazi kwenye nyaya za juu za umeme, na kazi yoyote iliyopatikana ya kufanya, kupata riziki yangu, sikuwa mzigo wowote kwa hao watu.

48 Nampenda Bwana, ndivyo hivyo, mnaona, si pesa, si vitu hivyo, ni ku—ni kujaribu kulifanya Kanisa la Mungu, na sisi sote pamoja, tupate kupaa juu katika Unyakuo huo mkuu. Ninaangalia mwisho, ndio ninaoangalia, kama nilivyowaambia kuhusu kuendesha baiskeli. Kama unaangalia *hapa* kile kinachoendelea sasa, bila shaka uta—utakimbia nje ya ubao, bali kama ukiendelea tu kuangalia mwisho, na kushikilia

imara, uendelee tu kuangalia mwisho, unaona, hutashikwa na wasiwasi sana, unaona. "Loo, *hili* litakuwaje? *Hilo* litakuwaje?"

49 Ninapoingia mkutanoni, wakati mwingine, ninawaona wavulana wangu, ninawaita, kundi langu, wataingia, "Ndugu Branham, hii ilienda . . . " Ninaendelea tu kuuangalia msalaba, mnaona, ninazidi tu kwenda, itakuwa sawa, ni sawa. Halijashindwa bado, kwa hiyo kamwe halitashindwa, hivyo tu. Mungu aliliahidi, wala haliwezi kushindwa, Mungu alisema hivyo. Na kwa hiyo tunampenda kwa ajili ya jambo hilo.

50 Sasa, tutasoma Maandiko, na tuwe tu na ma—maneno machache usiku wa leo. Ndipo kesho usiku, sasa, tutakuwa huko chini kwenye Ukumbi wa Manispaa. Nami ninasikitika kwamba—kwamba tulifanya maskini njia hii panda upesi sana, jinsi tulivyofanya, badiliko, hasa. Nafikiri, hao ndugu, baadhi yao walidhani labda ingewapa watu nafasi zaidi ili waweze kuhudhuria kanisa.

51 Nami natumaini ya kwamba hakuna mtu anayehudhuria makanisa haya mazuri hapa, ata—atakayekosa ibada zao kesho usiku, na—natumaini hawatafanya hivyo. Kama wana wajibu, simameni hapo. Kwamba msimame kwenye wajibu wenu kanisani mwenu, popote mwendapo, na kulipa zaka zenu mle, na kumpenda mchungaji wenu, na kumwombea. Na kama unahitaji kuombewa, mwombe, yeye ni mtu wa Mungu, atakuombea. Na Yeye atayajibu maombi yake, kama vile atakavyoyajibu yangu, ama ya mtu mwingine yeyote, maana hata hivyo, imani yako mwenyewe katika Mungu ndiyo inayofanya kazi, hiyo ni kweli, kweli hasa.

52 Sasa, ninyi nyote iweni wema, na Mungu daima awe pamoja nanyi. Nami natumaini kurudi pwani hapa tena, kutembelea huku chini tena kwenye kanisa hili dogo la Assembly of God, nije huku, nibishe mlangoni, natumaini mtaniruhusu niingie, nami nitaingia, niwahubirie tena, na tuwe na muda mfupi wa ushirika hapa. Nanyi mwaambie wachungaji wenu, na kadhalika huku, ninyi mnaozuru huku, wapeni upendo na salamu zangu, na mjaribu kumwelezea kile ninachojaribu kufanya, ni kujaribu kulishikilia Kanisa la Mungu aliye hai pamoja kama kitu kimoja, Mwili mmoja mkubwa. Naupenda wimbo huo:

> Hatujagawanyika,
> Sisi sote Mwili mmoja;
> Mmoja katika tumaini na Mafundisho,
> Mmoja katika upendo.
>
> Hima, twendeni enyi askari Wakristo!
> Wakienda kama vitani.

53 Na sasa, kadi za maombi zitatolewa kesho usiku saa kumi na mbili, kwenye Ukumbi wa Manispaa. Na sasa, juu ya hizo, sababu ya sisi kufanya hivyo, kuna umati mwingi sana ndani yake, halafu wanaanza kupigana kumbo, kusukumana, mmoja

akisema, "Nilikuwa hapa kwanza," mnajua jinsi ilivyo, hu—huwezi kufanya hivyo, inakubidi kuwapa kadi. Nayo hiyo kadi haina kitu ila namba ndogo tu juu yake, kwa hiyo wewe weka tu namba yako, ndipo namba yako ikiitwa, njoo huku.

54 Sasa, nafikiri hayo tu ndiyo yote niliyotaka kusema usiku wa leo, nami niliambia . . . Nao wanamuziki, huo wimbo, kwaya, na hao wote, ninawathamini, kila mmoja. Na kundi hilo lililoimba asubuhi ya leo, nini, ati Mwinyi? Mwinyi? Jamani, walikuwa waimbaji wazuri sana! Na maskini mama huyo hapo juu aliyeimba, alikuwa maskini mama mzuri, mdogo, alionekana kama maskini Mnorwe kwangu. Loo, kama yuko hapa, naye hayuko, sina nywele za kuvuta, kwa hiyo . . .

55 Mwajua, nilikuwa nikichanua zangu tatu ama nne nilizokuwa nimebakisha, hivi majuzi, naye mke wangu akaniambia, akasema, "Billy, unajua karibu una upara?"

Nikasema, "Lakini sijapoteza hata mmoja wazo."

Akasema, "Ati nini?"

Nami nikasema, "Sijapoteza hata mmoja wazo."

Akasema, "Naomba, niambie mahali zilipo."

56 Nikasema, "Hebu niambie zilikuwa wapi kabla sijazipata." Hiyo ni kweli. Hizo ni kitu halisi, sivyo? Kwa hiyo popote zilipokuwa kabla sijazipata, ziko huko zikiningojea niziendee. Kwa hiyo wakati mtu fulani anapowaambia Ndugu Branham amekufa, kamwe msiamini, nilikufa miaka mingi iliyopita, mnaona, ninaenda tu kwenye mwili ule mchanga kule. Wakati mzoga huu wa kale utakapokwisha:

Nitaanguka na kufufuka,
Niinyakue ile thawabu ya milele,
Na kupaza sauti, huku nikipitia hewani,
"Kwaheri, kwaheri, ewe saa tamu ya maombi!"

57 Vema, hiyo ni kweli, sivyo? Ni kweli. Mnaona, ninyi, hizo nywele zilikuwa kitu fulani, hazina budi kuwa ni kitu halisi, zilikuwa mahali fulani.

58 Mbona, niliwahi kuwazia hilo wakati mmoja, mimi ni mwaminio mashuhuri . . . Mimi, ninapiga risasi, mnajua jinsi ilivyo, na bunduki, na kadhalika, na watu hunipa bunduki, nami ninajipumbaza nazo. Mimi na Gene hapa, tuna ninii tu, tunajistarehesha tukilenga shabaha. Na—nami ninaweza kuchukua .220 Swift, hiyo ni moja ya bunduki zenye kurusha risasi kasi sana kutoka begani, na unaweza kutia risasi hiyo, kuitia hiyo risasi kwa mkono, kufikia futi elfu tano kwa sekunde. Sasa, wazia hilo. Unaona? Lakini ukitia tu robo moja zaidi ya baruti mle ndani, unaweza kupiga risasi moja kwa moja kwenye dirisha hilo, wala kamwe usingeigusa dirisha. Wala hakuna kitu kinachoanguka, hiyo risasi inarudi moja kwa moja kwenye gesi zake za asili, kama ilivyokuwa mamilioni ya miaka iliyopita.

Unaona? Sasa, mnaona, ilikuwa ni gesi, kisha ikawa kitu fulani, na ikidumu muda mrefu vya kutosha ingeweza kurudi moja kwa moja kuwa risasi tena. Mnaona? Hivyo ndivyo ilivyo. Mnaona?

59 Ni ninii yetu. . . Kile mimi. . . nywele hizi zilikuwako kabla hazijawa juu yangu, zinaningojea, na kila unywele umehesabiwa, wala hakuna hata sehemu yetu moja itakayopotea, lakini, "Nitaifufua katika siku za mwisho," asema Mungu. Ninaliamini hilo kwa kweli tu kadiri ninavyoamini nimesimama papa hapa.

60 Tumeumbwa tu kwa elementi kumi na sita, hizo ni petroli, potashi, nurulimwengu, na kadhalika, ili kwamba. . . Mungu anapata. . . iko duniani, na Yeye ataiita tu tena, nami nitajibu. Hiyo ni kweli. Ninaamini hilo. Ninaamini hilo kwa yote yaliyo moyoni mwangu, na nafsi, na nia, ninaliamini kwa uchaji juu ya Biblia hii, kama nikifa juu yake dakika mbili zijazo, ninaamini kwamba, kwamba Yeye ataita, wala hakuna hata kitu kimoja ambacho ni—ambacho nilikuwa nilipokuwa na umri wa miaka ishirini, ila nitakachokuwa Huko, hiyo ni kweli, kutokufa tu, haitanilazimu kufa tena.

61 Hilo si litakuwa zuri sana? Wazieni juu ya watu wakongwe. Nalo ono hilo, nilipokuwa Kule, nilimwona mwanamke huyo, wanawake warembo kuliko wote niliopata kuwaona, nywele ndefu kufikia viunoni mwao, wamevaa sketi ndefu, wakinikumbatia kwa mikono yao, wakiniita ndugu. Niliwaona wanaume, na meno yao meupe kama lulu, macho yao yakimetameta, wakikimbia na kunikumbatia kwa mikono yao, wakiniita ndugu, wote ni vijana. Wala nisingeweza kulielewa.

Naye akasema, "Unamwona mwanamke yule aliyekukumbatia hivi punde?"

"Naam."

Kasema, "Alikuwa amepita umri wa miaka tisini ulipomwongoza kwa Kristo. Kwa nini asikuite ndugu yake mpendwa?"

Hilo linanifanya kukaza mwendo. Loo, jamani! Mnaona ni kwa nini ninakatata na kuvuta, "Hima, twendeni, marafiki"?

62 Chini moyoni mwangu nina siri nyingi, mnajua hilo, mnajua hilo kabisa, kwa hiyo inawabidi tu kuniamini katika kuwaongoza, siliachi Neno kamwe, nitadumu moja kwa moja na Neno, bali ninyi jipimeni tu moja kwa moja Nalo sasa.

63 Ndipo mnaporudi hapa, mnaporudi kanisani, njoni mkaninii, kama nikija, Bwana akitujalia kuishi, na Yesu akikawia, mwaka mmoja tangu leo nitarudi, ninatumaini kuona umati huu hapa ukiangaza tu kwa ajili ya utukufu wa Mungu na nguvu za Mungu, kisha mseme, "Unajua nini? Kila Assembly of God, kila Church of God, kila Foursquare, kila Umoja, Uwili, Utatu, na Unne, na kote huku na huku pwani wako tu katika

moyo mmoja, na uamsho huu uko katika nguvu za Mungu, ukiitikisa tu pwani hii jinsi ambavyo haikutikiswa kamwe."

Loo, ningesema, "Bwana, mruhusu mtumishi Wako aondoke kwa amani, kwa kuwa macho yangu yameuona wokovu Wako." Hiyo ni kweli, ningekuwa tayari kwenda.

Kama mnayaandika Maandiko chini . . .

Mnapendeza sana. Billy ananiambia, kasema, "Baba, unazungumza muda mrefu kuliko unavyohubiri," akasema.

64 "Vema," nikasema, "nina jambo la kuzungumzia, kwa hiyo, na jambo fulani ambalo ni zuri, jambo ambalo ninalipenda sana." Nami najua sote tunalifurahia, sivyo? Kuendelea kuzungumziana sisi—sisi kwa sisi.

65 Sasa, ninataka kuninii . . . nina Maandiko yaliyoandikwa hapa usiku wa leo, pia, huenda nikayarejea. Nami nawatakeni mfungue Yeremia 8:22, nasi tutasoma kifungu hivi—vifungu hivi:

> *Je, hapana zeri katika Gileadi; huko hakuna tabibu huko? mbona basi . . . haijarejea afya ya binti ya watu wangu?*

66 Hilo ni swali, liweke hilo moyoni mwako. Swali: "Je, hapana zeri? Je, hapana zeri katika Gileadi; huko hakuna tabibu? Basi mbona haijarejea afya ya binti ya watu Wangu?" Kama hakuna zeri, wala tabibu, kama ipo, basi mbona—mbona hajapona? Ndilo swali.

67 Ninaamini kama Mungu akifanya maandalizi, na njia ya kuepukia kwa ajili ya watu Wake, akiwafanyia watu Wake jambo fulani, halafu watu wakatae kulipokea, Yeye ana haki ya kuuliza kwa nini.

68 Vipi kama ulimfanyia mtu jambo fulani? Kama ukisema, "Sasa, nitakupa motokaa yangu, imejaa petroli, iko katika hali nzuri ya kuendeshwa, nataka unichukue huko pembeni katika dakika kumi." Nawe ungojee mchana kutwa na usiku kucha, wala mtu huyo haji kamwe, kisha ukutane nao mahali fulani una haki ya kusema, "Mbona hukufanya hivyo?" Hiyo ni kweli?

69 Naye Mungu katika nyakati zote, wakati alipofanya . . . Kamwe hajafanya njia ya kuepukia ambayo watu wote wangeipitia, daima kumekuwa na wale waliojiondoa. Lakini ninawatakeni mwone jambo moja kuu, kwamba daima Mungu hutuma rehema, nayo hukumu hufuata rehema. Na wakati wewe, usipoikubali rehema, basi huna budi kupokea hukumu. Unaamini hilo?

70 Sasa, kama ukiangalia, kabla tu ya Vita vya Kwanza vya Dunia, walipokea ubatizo wa Roho Mtakatifu katika nchi hii, na nchi zingine. Mnaona? Sasa, tulipoona jambo lililo kuu sana, ule uamsho ulio mkuu kuliko yote, huduma kuu sana zilizopata kujulikana tangu siku za Yesu Kristo, zimepitia katika taifa hili, niambieni ni lini, ni wapi, ni mahali gani tuliwahi,

tulipopata kamwe kusoma katika kitabu, ama kusikia, ama hata kujua huduma kama tuliyo nayo leo hii. Sasa, ni kitu gani kitakachoifuata? Hukumu, kuikataa.

71 Angalieni huduma ya Bwana wetu, kwa sababu waliikataa, tulikuwa nalo katika ibada jana usiku, kwa kuikataa, ilikuwaje? Hukumu ilifuata. Hakika, daima. Kwa sababu wao . . .

72 Tazama, Roho Mtakatifu alishuka Urusi yapata miaka mia moja iliyopita. Mlijua hilo? Bila shaka, alishuka. Wakamkataa. Walipata nini? Alishuka Ujerumani kabla hajashuka hapa. Walipata nini? Hawangeukubali msalaba, kwa hiyo wakapata misalaba miwili, swastika. Mnaona?

73 Na sasa, kwa sababu tulikataa, kama taifa (Nami kwa kweli ninaamini tulifanya kosa letu baya sana katika mwaka wa '56. Na wakati sisi . . . Sasa, kumbukeni, nimeliandika kwenye kumbukumbu, mnaona.), nanyi kumbukeni tu, kamwe hatarudi tena, limekwisha. Hiyo ni kweli. Tunaokota masazo. Lakini kamwe halitarudi tena, kamwe hakutakuwa na uamsho mkuu utakaoenea katika taifa hili kabla ya hukumu. Linaingia hukumuni, liko njiani kwenda huko sasa, karibu wakati wowote litawasili. Mimi, mwenyewe, ninaamini ya kwamba kabla hukumu hii kuu haijalipiga taifa hili, ya kwamba Kuja kwa Pili kwa Yesu kutaliondoa Kanisa Lake duniani, ninaamini hilo.

74 Sasa, tunajua ya kwamba ulimwengu hauwezi kustahimili mlipuko wa atomiki. Mungu ametufanyia njia ya kuiepuka, bali kama tukikataa kuikwepa, basi Yeye atauliza ni kwa nini hatukuipokea.

75 Sasa, Yeye amefanya kila kitu alichoahidi katika Biblia. Sasa, watu wengi . . . Sitofautiani na wasomi, la, bwana, bali mimi hufanya kazi tu kwa ufunuo, huo ufunuo hauna budi kuwa ni Neno, kama si kulingana na Neno, basi ni ufunuo mbaya. Wengi wanatazamia mambo makuu kutukia, nao wanayaelekeza hayo huko Israeli wala si Kanisani. Hebu chukueni sura tatu za kwanza za Ufunuo nawe una Kanisa papo hapo. Ndipo Yohana alinyakuliwa kutoka kwenye wakati wa kanisa. Sasa, kwa hiyo siku yetu karibu imekwisha, Kanisa, Injili sasa itarudi kwa Wayahudi huko Palestina. Na ndipo wakati wa Mataifa umekwisha, kadiri ulivyo wakati wa kanisa, lile Kanisa halisi, lililojazwa na Roho.

76 Mungu anapofanya njia, wala watu hawatembei humo, Yeye anasema, "Kwa nini?" Wakati mmoja mfalme wa Israeli, kwa sababu siku moja alikuwa akitembea kwenye madirisha ya baraza lake, ndipo akaanguka kupitia hilo dirisha, naye, ikamwumiza, akashikwa na ugonjwa kutokana nayo, na kwa hiyo akalala kitandani mwake. Basi akiwa ni mfalme wa Israeli, hata hivyo badala ya kutuma mtu akamtake Mungu shauri, aliwatuma baadhi ya watu wake huko Ekroni kuuliza kwa

Baalimu, Beelzebuli, ile miungu kule juu, manabii wao, kama atapona au la.

77 Sasa, mnajua Mungu huwafunulia manabii Wake siri Zake, tunajua hilo, kwa watumishi Wake, Yeye hufunua hizo. Naye Eliya labda alikuwa amerudi kule pangoni mwake. Naye alijuaje ya kwamba mfalme aliwavuta watu hawa ndani, akawachukua watu wawili ama watatu, na kusema, akawaagiza, na kusema, "Sasa, vukeni taifa letu, itawachukua siku kadhaa, mshuke mwende Ekroni, na mtakapofika kule chini, kutakuwako, mtakutana na Baali, mu—mungu wa—wa Ekroni, na sasa, mumtake shauri nabii wake apate kumwuliza Baalimu, kama nitapona au la"?

78 Lakini mnajua, kwa kuwa alikuwa Mwisraeli, basi Mungu alimfunulia nabii Eliya, Naye akasema, "Kwea, ukasimame njiani, ukawasimamishe."

79 Na kwa hiyo, askari hawa, ama walinzi wa hekalu wakaja, wakitembea barabarani, wakizungumza, wakiwa na agizo kali la kupanda kwenda kumtaka shauri mungu wa kipagani kuhusu jambo hili, kwa sababu taifa lote lilikuwa limeingia katika dhambi.

80 Na hiyo ndiyo shida siku hizi, taifa lote linaingia dhambini, vilabu vya wiski, watu wakiingia baridi na kuwa wa kawaida, kwenye vipindi vya redio visivyokaguliwa, vipindi vya televisheni visivyokaguliwa, na inavutia sana, na dhambi inapendeza sana, mpaka inavutia usikivu wa watu. Na kama kweli hawajazaliwa mara ya pili, ambapo mvuto wao uko kwa Kristo na kwa nia moja, watafuatilia upuuzi huo, watatenda kama watu hao. Na ro—roho ya hayo itawaingia.

81 Ilikuwa kwamba Wapentekoste wa kale wasingewaruhusu watoto wao hata kwenda kwenye sinema, ibilisi akayafunika macho yao, akaleta sinema moja kwa moja nyumbani. Hiyo ni kweli. Na kwa hiyo, mnaona jinsi alivyoileta? Mjanja, mwenye busara, mwenye hila awezavyo kuwa. Kamwe usimdharau, wewe kaa hapo msalabani, mahali pekee pa kukaa upate usalama.

82 Kwa hiyo wale wazee wa kale, mnaona, walidumu na Mungu, nabii huyu alidumu na Mungu, kwa hiyo Mungu angeweza kuzungumza naye. Kwa kawaida, watu huenda kama taifa liendavyo, daima wamefanya hivyo. Na hiyo ndiyo shida siku hizi, watu wanaenda kama taifa liendavyo, kama ni sawa, taifa linahalalisha unywaji pombe, mbona, ni sawa. Wakihalalisha . . .

83 Nilimwona mama mmoja akitembea mtaani hivi majuzi, ambapo askari yeyote aliyekuwa na adabu yoyote, angemfukuza msichana huyo barabarani, jinsi alivyokuwa amevalia, sijapata kuona kitu chochote kichafu hivyo maishani mwangu mwote. Watu wakikimbia kutoka kwenye kituo cha petroli na kadhalika, wakimtazama kipumbavu msichana huyu barabarani. Uadilifu wa watu wetu umeenda wapi jamani? Mungu alimheshimu

mwanamke kuwa mmoja wa johari za dunia. Na jinsi atakavyojiuza kwa—kwa ibilisi ni zaidi ya . . . Vema, ni kwa sababu yeye hamjui Mungu, ni hayo tu. Mnaona? Twajua ya kwamba mwili wake ni mtakatifu, naye hapaswi kufanya hivyo, nao wanafanya hivyo kwa vyovyote vile, kwa sababu wanafikiri ni sawa. Riki, na Elvis, na hao wote, wanavutiwa tu na hayo, na, "*Wheet-whew* !" miluzi ya mbwa, nao wanafurahia hiyo. Hiyo inapaswa kuwa fedheha kwa mwanamke yeyote, mmoja wao akimpigia mbinja namna hiyo.

84 Naam, wewe ni mwana-kondoo, unapaswa kuwa; mpenzi na mke wa mwamume fulani, mama wa mtoto fulani mchanga, unapaswa kuona aibu kufanya mambo kama hayo. Uadilifu wa uwanawake halisi unapaswa, he—heshima uliyokuwa nayo kwa mama yako inapaswa kukuongoza vinginevyo. Hiyo ni kweli.

85 Angalieni jinsi ambavyo imekuwa tu . . . Nao wahubiri wanaachilia tu, wanaliacha liingie moja kwa moja kanisani mwao. Hatimaye, linanyemelea tu polepole, kidogo namna *hii*. Niliketi na kuzungumza na maskini mhubiri wa Kimethodisti si muda mrefu uliopita, alizoea kuimba wimbo:

Tulilegeza kamba, tulilegeza kamba,
Tukapatana na dhambi.
Tulilegeza kamba, kondoo wakatoka nje,
Lakini mbuzi waliingiaje?

86 Vema, nafikiri wimbo wake kweli unaelezea jambo hilo, mlilegeza kamba, hivyo tu. Kalegeza tu kamba, mmoja akaingia, naye akaanza kulizungumzia *hivi*, na—nao wakaanza kuangalia, akafanikiwa kidogo, kisha kasema, "Vema, kama Jones anaweza kufanya hivyo, Dk. Jones, naweza, pia," na muda si muda mwajua hiyo hapo inaenda.

87 Na ni kama tu ile sleji ya kale ya kutelezea, unateleza kote nayo. Ni wangapi wanaokumbuka ile sleji ya kale ya kutelezea? Uliketi chini, ukaendelea kuteleza kwa urahisi sana, ukiona jinsi unavyokaribia ukingoni, na kadhalika, kabla hujajua, [Ndugu Branham anadata vidole vyake—Mh.] huyo ukaanguka. Hilo ndilo lililotukia kwa kanisa la Kipentekoste, hiyo ni kweli. Usione jinsi unavyoweza kuikaribia zaidi, angalia jinsi unavyoweza kukaa mbali, nayo.

88 Wakati mmoja kulikuwa na dereva aliyepaswa kupanda mlima, naye huyo mtu ilimbidi kuharakisha na kuvuka milima, na kwa hiyo wakasema . . . dereva mmoja akaja, akasema, "Mimi ni dereva mzuri sana, ninaweza kuendesha farasi hawa sita na mkokoteni wangu ndani ya inchi sita kutoka kwenye ukingo huo, kwenye ukingo huo mkubwa wa futi elfu moja. Ninaweza kuliendesha kwenye inchi sita kwa shoti kamili, na kamwe nisianguke."

Ndipo huyo dereva mwingine akasimama, akasema, "Bwana, hebu nikupeleke, ninaweza kuendesha umbali wa inchi nne kwa mwendo wa kasi, na kamwe—na kamwe nisianguke."

Basi kulikuwako na mzee mmoja amesimama tu pale akiangalia, yule dere-. . .huyo mtu alitaka kuvuka mlima, kasema, "Na wewe je, bwana?"

Akasema, "Vema, angalia, bwana, kulingana na yale wanayozungumzia, wao ni madereva bora kuliko nilivyo mimi. Mimi huukumbatia ukuta, sibahatishi hata kidogo."

Akasema, "Wewe nivushe." Mnaona?

89 Usione jinsi unavyoweza kuikaribia dhambi bila kutenda dhambi, angalia jinsi unavyoweza kukaa mbali nayo, hivyo ndivyo ilivyo. Ondoka kwenye eneo hilo kabisa. Hivyo ndivyo ninavyolitaka kanisa, hilo ndilo kanisa ninalotaka kuwa mfuasi wake, lile linaloepukana na hata mwonekano wenyewe wa dhambi, kaa mbali nayo.

Unasema, "Vema, wasichana wetu, ama wanaume wetu, ama nanii wetu. . .wana maskini burudani ndogo safi tu." Loo, jamani, jamani, "ati burudani safi," kile Wamarekani wanachokiita "burudani safi," hmm!

90 Nilikuwa huko Canada si muda mrefu uliopita pamoja na rafiki yangu mwema Fred Sothmann, aliyeketi pale. Moja ya makundi mashuhuri sana Marekani, sitataja jina la kundi hili, na kwa hiyo, walikuwa huko juu wakiwa na m—mkutano mkuu, na chupa za wiski zimelundikana juu ya kila kitu. Nilipoingia usiku huo, nikaanza kupanda juu ya—ya, nilipoingia kwenye lifti, basi mvulana huyo, hata ilinifanya nione aibu kwamba nilikuwa Mmarekani, basi aliangalia pale, naye. . .Ni—nikasema, "Kwani kuna nini?"

Akasema, "Wamarekani wameingia ndani usiku wa leo."

Nami nikasema, "Jamani!" Hiyo ilikuwa huko Saskatoon. Nami nikasema, "Ni chama fulani kikifanya mkutano wao mkuu."

91 Na kwa hiyo, nilipofika kule juu na kutoka ukumbini chumbani mwangu, nikaanza kushuka, kulikuwako na wasichana wawili wamesimama kule nyuma, wote wawili wamevaa pete za arusi pamoja na ninii zao, wamevaa tu sketi zao za ndani, wamelewa kupindukia. Nao maskini wanaume walevi wakijaribu kuwafuata, labda mume yuko nyumbani, akiwachunga watoto, labda wanaume hawa, wakiwafuata hawa wasichana, huku wake zao wakiwa nyumbani wakimtunza mtoto mchanga, lakini walikuwa na maskini burudani ndogo safi ya Kimarekani. Ni uchafu na dhambi! Hiyo ni kweli.

92 Nao wakashuka ukumbini, naye maskini jamaa huyu akamshika huyu kwa sketi ya ndani, na kujaribu kumvuta, na nusura akate moja ya kamba kutoka begani, naye akaanikwa,

vibaya sana. Akashuka, wasichana warembo, wote wawili, wakashuka kupitia pale, wakiyumbayumba namna *hiyo*.

Nami nikarudi tu kwenye chumba kidogo, kitu kama, ukumbi mdogo namna *hii*, na kuangalia.

93 Walikaribia sana mbele yangu, walikuwa na chupa ya wiski, naye akanyosha mkono, akachukua chupa hii, na kuiinua juu, kisha akanywa pombe nyingine, pete hiyo ya arusi iking'aa mkononi mwake.

Moyo wangu ulinitoka tu, nami nikawazia, "Maskini msichana wa kupendeza namna hiyo, halafu angalia kile anachofanya!"

94 Ndipo huyo mwingine akapita pale, akashika—akashika maskini sketi hii, ile aliyokuwa amevaa, sketi yake ya ndani, akaivuta juu kadiri alivyoweza, kisha akapaza sauti, "Hoyee, haya ndiyo maisha!"

95 Nikatoka nje ya huo ukumbi, nikasema, "Samahani, hiki ni kifo! Hii ni mauti! Biblia ilisema, 'Yeye anayeishi katika anasa amekufa ingawa yu hai.'"

Wakasema, "Karibu pombe."

Nikasema, "Hebu kidogo. Mimi ni Mmarekani."

"Vema," wakasema, "maskini Yankee!"

96 Nikasema, "Ngojeni kidogo, mimi ni mhubiri wa Injili. Hivi hamjionei aibu?" Nikasema. Mmoja wao alikuwa mwalimu wa Shule ya Jumapili. Nikasema, "Hivi hujionei aibu?" Nami nikamshika mkono, alikuwa mdogo sana asingeweza kukimbia, nikamshika. Akaanza kupiga mayowe, na kujivuta namna *hiyo*, nami nikafikiri labda wangetoka na kunikamata, waniwazie mabaya. Kwa hiyo nikasema, "Hivi—hivi hujionei aibu? Kama wanawake hapa juu, nyote wawili mmevaa pete za arusi nao waume zenu wako nyumbani!"

Kasema, "Tuna maskini burudani ndogo tu safi."

Nikasema, "Ni dhambi!" Kweli.

97 Mungu alifanya njia ya kuepukia bali kamwe hawataichukua. Ni kitu gani kinachowafanya watu kufanya hivyo? Ni kwa sababu Mungu alimwumba mwanadamu apate kuona kiu. Nawe. . .Mtu yeyote anathubutuje kujaribu kuridhisha hiyo shauku takatifu kwa mambo ya ibilisi! Usijaribu kufanya hivyo, kamwe hutaridhika, inaleta tu huzuni, itakufanya uchukue bastola na kulipulia mbali akili zako. Hilo halina uhai halisi ndani yake, uhai halisi hutoka kwa Mungu. Kamwe huwezi kuridhika na kuwa na furaha kabisa . . .

98 Na mmoja wa hawa Wakristo nusu, wanaodhaniwa kuwa, ndiye mtu mwenye mashaka sana ulimwenguni. "Loo, siwezi kufanya jambo *hili*. Kama kanisa langu lingejua nilifanya *hivyo*!" Mungu anajua unafanya hivyo, inaleta tofauti gani? Papo

hapo, uweke moyo wako wote moja kwa moja kwa Mungu, na udumu moja kwa moja nao, ndipo una furaha, ukitembea kwa amani pamoja Naye.

99 Eliya akapanda juu, akasimama barabarani, hawa hapa watu hawa wanakuja, na kusema, wakamjia, akasema, "Rudini mkamwambie mfalme wenu, BWANA ASEMA HIVI: hatoki kwenye kitanda hicho. Mwulizeni mbona hakutuma mtu huku chini, yeye ni Mwisraeli. Je, ni kwa sababu hakuna Mungu katika Israeli? Ni kwa sababu hatuna nabii? Israeli haina nabii, wala Mungu? Kwa nini utume mtu huko Ekroni? Hivi Israeli haina nabii? Hivi Israeli haina Mungu? Basi mbona utume mtu kwa Beelzebuli, ama kwa—ama kwa Baalimu? Kwa nini utake shauri mambo hayo? Ni kwa sababu hatuna nabii yeyote, ama Mungu yeyote?"

100 Hivyo ndivyo Mungu atakavyouliza Marekani moja ya siku hizi, "Kwa nini mkafanya mambo hayo?" Hivyo ndivyo Mungu atakavyoliuliza kanisa la Kipentekoste moja ya siku hizi, "Kwa nini mlienda kwenye madansi? Kwa nini mlitenda hivyo? Kwa nini wanawake wakakata nywele zao? Kwa nini wanaume wakafanya mambo *haya*? Kwa nini walivalia kama ulimwengu? Kwa nini walitenda kama ulimwengu? Je, ni kwa sababu hapakuwapo na Injili, hakuna furaha, hakuna Roho Mtakatifu aliyemwagwa juu yenu? Ni kwa sababu hawakuwa na mhubiri ambaye angeliihubiri?"

101 Loo, ni kwa sababu, kama tu ilivyokuwa katika siku za mfalme, ilikuwa ni ukaidi wake mwenyewe, alimchukia huyo nabii, maana mama yake alimchukia, alikuwa ni mwana wa Yezebeli. Na hiyo ndiyo sababu Ahabu, mwaminio mkwamia mpakani. . .Na hiyo ndiyo sababu ilikuwa, alitoka kwenye kanisa la kale, baridi, la kawaida. Na hiyo ndiyo sababu kwamba alimchukia nabii, kwa sababu nabii alimwambia ukweli, naye hakulichezea, naye akamchukia. Mama yake alimchukia nabii huyo, baba yake alimchukia nabii huyo.

102 Baba yake alisema, wakati—wakati Yehoshafati aliposhuka, na kushuka kwenda kule kuketi pamoja na Ahabu, alisema, "Hebu twende hapa juu Ramoth-gileadi na kuiteka ile nchi kule juu," kasema, "ni mali ya Israeli."

103 Na, bila shaka, alimwonyesha mambo yote makuu ambayo—ambayo walikuwa nayo, naye, bila shaka, hivyo ndivyo ibilisi afanyavyo, kukuonyesha mambo yote makuu, nayo yakayapofusha macho yake, naye akasema, "Vema, watu wetu ni watu wako." Kasema, "Lakini hivi hufikirii inatupasa kumtaka shauri Bwana juu yake kwanza?"

104 Akasema, "Hakika, bila shaka, Yehoshafati, hiyo ni kweli kabisa, inatupasa. Nina wahubiri mia nne wa seminari hapa chini, walio bora kuliko wote," walikuwa na walio bora kuliko

wote nchini. “Loo, nitaenda niwachukue wote, niwalete hapa juu.”

Nao wote wakatabiri kwa nia moja, kasema, “Kwea, kwea, Bwana yu pamoja nawe.”

Lakini hilo halikumfaa Yehoshafati vizuri, akasema, “Hivi huna mmoja zaidi?”

“Ati mmoja zaidi? Wakati tukiwa na mia nne kutoka seminari yangu wakiwa na moyo mmoja, kila mmoja akinena jambo lile lile!”

Sijali ni wangapi wanaonena, kama si Neno la Mungu, si Neno la Mungu!

“Tuna manabii mia nne werevu, waliofunzwa, wenye elimu wakisimama hapa, kwa moyo mmoja wanasema uende.”

Lakini Yehoshafati akasema, “Lakini, hakika, una mmoja zaidi.”

105 Akasema, “Naam, tuna mtakatifu mwingine anayejibingirisha,” samahani, huenda sikupaswa kusema hivyo, lakini, vema, tayari nimelisema, kwa vyovyote vile. “Naam, tunaye mmoja, Mikaya, mtakatifu anayejibingirisha hapa juu, bali ninamchukia.” Haya basi.

“Loo, mfalme asiseme hivyo.” Kasema, “Pandeni mkamwite, mwone atasema nini.”

Akasema, “Ninakuonya, yeye hutabiri tu mabaya dhidi yangu.”

106 Hakika, angewezaje? Angeweza kufanya nini zaidi? Wakati ameona, mambo ya ulimwengu, angeweza kufanya nini ila kuitetea kweli?

107 Wakaenda wakamchukua, halafu basi, bila shaka, wakaagiza halmashauri ya mashemasi kwenda kumfanya afanye uamsho huo, kisha kasema, “Sasa, ngoja kidogo, sasa usihubiri dhidi ya *hili*, wala usihubiri dhidi ya *hilo*. Usiwaambie wanawake hawapaswi kukata nywele zao, wala usiwaambie hawapaswi kujipodoa, maana wanawake wetu wote hufanya hivyo.”

Nimewafanya kusema hivyo, nami ninasema, “Nyamazeni! Mnanitaka—mnanitaka, mimi huyu hapa naja.” Unaona?

108 Kwa hiyo, wakamwambia Mikaya, wakasema, “Sasa, wewe sema jambo lile lile hao wengine wanalosema, kwa sababu siku moja, unajua nini, utakuwa mwangalizi mkuu, kama tu utanisikiliza, ni—nitaninii . . . watakupeleka kwenye kongamano kama tu utakubaliana nao.” La, hilo halimo katika moyo wa nabii halisi wa Mungu. La, bwana.

109 Hakuwa akitaka kukubaliana nao, hakuwa na mchezo, wala risiti za mlo wa kununuliwa. Kwa hiyo, yeye akasema tu, “Nitasema tu yale Mungu anayoweka kinywani mwangu

kusema, ni hayo tu." Kwa hiyo, akashuka kwenda kule na kusema, "Nipeni usiku wa leo, hebu nione kile Bwana atakachosema." Akarudi kesho yake, mnajua kile alichosema, "Niliwaona Israeli milimani, wametawanyika kama kondoo wasio na mchungaji."

Kasema, "Nilikwambiaje?"

110 Ndipo kiongozi wa Shirika la Wahudumu akampiga kofi mdomoni, akamwangusha chini kabisa. Naam, hiyo ni kweli. Kasema, "Roho wa Mungu alipitia njia gani alipotoka ndani yangu?"

Kasema, "Utaona wakati unabii wangu utakapotimia."

111 Akasema, "Mtieni katika gereza la ndani, mrudisheni huko ndani, na kumlisha chakula cha huzuni na maji ya huzuni," Ahabu akasema, "hata nitakaporudi kwa amani."

Mikaya akasema, "Ukirudi kamwe, Mungu hajasema nami."

112 Sasa, kwa nini wachukue . . .? Kwa nini hawakuchukua neno hilo la mtu mmoja? Mnaona? Mtu mmoja katika taifa zima akisimama dhidi ya makosa. Nao hao wengine . . . Kwa nini? Kwa sababu waliamini kundi lile maarufu. Wanaamini Ph.D., ma-LL.D., na ma-Q.S.D., na kila namna ya *ma-D.D.* na za kila namna, kila kitu kiliambatana nalo. Walitaka kuliamini kwa sababu walidhani hao walikuwa werevu zaidi, na wenye elimu.

113 Lakini angalieni, ni nani aliyekuwa sahihi? Mikaya alikuwa sahihi, kwa sababu alidumu kabisa na Neno la Bwana, alidumu sawasawa kabisa. Angewezaje kubariki kile Neno la Mungu lilikuwa limelaani?

114 Ninawezaje kuwaambia ninyi wanawake mko sawa mkiwa na nywele fupi, na kujipodoa, na nguo kana kwamba mlikuwa mmemiminiwa mle kama soseji iliyotolewa ngozi, na kitu kama hicho hapa nje, wakati Neno la Mungu linalihukumu? Kwa nini siwezi kuwaambia mko sahihi, Assemblies of God zenu, na Churches of God, na Foursquare, na kuwaingiza watu, *kujiunga*, wakiingia namna hiyo, kuwafanya watende kama ulimwengu, na kuendelea, mkiwa na vitu mbalimbali vya kila namna, wakati ni makosa? Kweli, ni makosa. Tunachohitaji si ufuasi mpya, ni nguvu za Roho Mtakatifu kurudi kanisani tena, uamsho wa Kipentekoste wa mtindo wa kale katika nguvu na madhihirisho ya Roho Mtakatifu. Tumetosheka na upuuzi huu!

115 Kanisa la Foursquare ni mojawapo wa wadhamini wangu wakuu, wana baadhi ya watu walio wazuri sana mle ndani, Dk. Teeford, wengi wa hao, wao ni watu watauwa kwelikweli. Lakini wakati mimi, na Dada McPherson, na Rolf tulipokuwa tumeketi tukila siku moja, tulipokuwa tukizungumza juu ya shirika fulani, ama mtu fulani katika pwani hii aliyekuwa amewachukua karibu wafuasi wao wote, nilisema, "Hilo linawanena vibaya sana." Kwa nini waende ambako wanaenda

kusema wajenge kanisa la dola milioni nne ama tano, na tayari umejenga lako, huko wapate kulipia deni hilo?" Nikasema, "Ilikuwaje?

116 "Mnajua nini?" Nikasema, "Wakati Dada McPherson alipokuwa hapa alikuwa na uamsho, alidumu na Roho, watu wangekuja kutoka kila mahali, waliojazwa na Roho Mtakatifu. Lakini ilikuwaje wakati alipokufa? Mlianza kufanya ma-Ph.D., ma-D.D.D., ma-L maradufu D., ma-Q.S.D. na kila namna ya vitu. Basi mna nini sasa? Mjengo wa thamani ya dola milioni moja usio na faida mikononi mwenu." Hiyo ni kweli. Tunachohitaji ni kurudi kwenye ujumbe wa Kipentekoste, kumrudia Roho Mtakatifu, hiyo ni kweli.

117 Mikaya asingeweza kusema zaidi ya hayo, kwa sababu hivyo ndivyo Eliya alivyosema. Akasema, "Niliona jeshi la Mbinguni wote wamekusanyika pamoja wakifanya baraza, Na Yeye akasema, 'Tumtume nani ashuke aende akamdanganye Ahabu?'" Kwa maneno mengine, kufanya neno la nabii Eliya litimie, kumpeleka huko nje kusudi aweze kuuawa, kwa sababu mbwa hawana budi kuiramba damu yake kwenye gari, maana Eliya alisema hivyo, hilo lilikuwa ni Neno la Mungu. Mungu akasema, "Tumtume nani akafanye hivyo?"

118 Naye akasema pepo wa uwongo alitokea, akasema, "Nitashuka niende nikawaingize hao wahubiri wote, nami nitawafanya wadhanie wako sahihi."

119 Kwa nini? Angewezaje kufanya hivyo? Roho wa uongo angewezaje kuingia ndani ya mhubiri? Kwa sababu alikuwa amepatana juu ya Neno la Mungu. Kama angehubiri Neno la Mungu, asingelimwingia. Roho yeyote anayenena kinyume na Neno hilo, ni uwongo. Hiyo ni kweli. Hiyo ni Urimu na Thumimu ya Mungu. Kweli. Kama haliko *Hapa*, ni kosa, *Hili* ndilo.

120 Mungu wetu anaweza kufanya mambo ambayo hayajaandikwa katika Kitabu hiki, lakini Yeye anayo mengi ya kutosha hapa kwangu mimi kudumu nayo kujua ya kwamba niko sahihi, papa *Hapa*. Kama nikiweka *Hili* tu, hilo litakuwa sawa.

121 Sasa, "Nenda, umwambie, yeye hatoki humo kitandani, BWANA ASEMA HIVI, hatoki kitandani, atafia kitandani," naye akafa.

122 Kwa hiyo wakati wale wajumbe waliporudi kwa Mfalme Ahazia, yeye alisema, mwana wa Ahabu, kwa hiyo akawaambia, akasema, "Mnafanya nini kurudi mapema hivi?"

123 Akasema, "Tulikutana na mtu huko juu aliyesema, tukwambie, 'BWANA ASEMA HIVI, mbona ukatuma watu kule? Je, hakuna nabii katika Israeli wa kumtaka shauri? Hivi hakuna Mungu huku chini katika Israeli, inakubidi kutuma watu huko kwa makafiri?'"

124 Kwa maneno mengine, "Hivi hakuna furaha ya kutosha Kanisani? Mbona mnakaa nyumbani Jumatano usiku kuangalia televisheni? Hivi hakuna furaha Kanisani tena, hakuna kitu moyoni mwako kinachotamani kusikia Neno la Mungu kuliko kinavyopenda kutazama *Tunampenda Susie*, ama chochote kile ambacho unakaa nyumbani kutazama?"

125 Kuna nini? Wachungaji kamwe hawakuniomba niseme jambo hili, ninawaambia tu ukweli. Kanisa lina shida gani? Hiyo ndiyo shida hasa. Kama ninyi watu mkisema, "Vema, mchungaji wetu. . . " Mchungaji wetu bure! Ninyi jipatanisheni na Mungu, naye itambidi kufanya hivyo, la sivyo ataondoka. Hiyo ni kweli. Hebu kanisa lijiweke sawa. Hiyo ni kweli. Dumumi tu na Neno. Hivi mmepoteza furaha yote? Injili haisikiki kwenu kama ilivyokuwa? Kuna kasoro basi. Kama upendo huo wa Mungu hauko juu ya kila kitu kingine. . . Moyo wako, wakati kengele hiyo ya kanisa inapolia, moyo wako unawaka tu.

126 Hapa miaka kadhaa iliyopita nilikuwa nikishuka kwenye nguzo ya simu, nami nilikuwa nikifanya kazi katika mashirika ya umma nilipokuwa mchungaji wa maskani ya Kibaptisti. Na—naye Dk. Brown ni rafiki yangu msiri sana, ni mfuasi wa kanisa zuri la kimadhehebu kule, nao wanasema wana wafuasi mia tano, lakini wako kote ulimwenguni, na baadhi yao wamekufa kwa miaka mingi, lakini, kwa hiyo hata hivyo, alisema hao ndio waliokuwa na kadi zao.

127 Kwa hiyo, basi nilikuwa nikishuka kwenye nguzo, na—nami nilikuwa chini ya kilima chini ya New—New Albany kule, nilikuwa nimeshuka kwenda kuchukua bili ya umeme. Walikuwa wameniambia, niende kule juu na kuwaambia hao watu walikuwa wameachilia ile bili ya umeme iongezeke kwa muda mrefu walivyoweza, walikuwa wamepewa notisi nyekundu, nasi ilitubidi kwenda kuuzima umeme.

128 Vema, badala ya kupanda juu na kuuzima, niliwazia, kama muungwana, ningeenda mlangoni na kubisha mlango na kumwambia huyo mama kitakachotukia. Nikaenda mlangoni, nikabisha mlango. Kulikuwako na maskini mwanamke mmoja, msichana, aliyekuja, pale akiwa hana nguo za kutosha kuishindilia bunduki ya marisau, alikuja pale, mwajua, vema, ungeweza kuzipakia kwenye kasha la kiberiti, kweli, sijawahi kumwona mwanamke aliyevalia pungufu hivyo maishani mwangu.

Akaja mlangoni, nilikuwa, niligeuza tu kichwa changu, nikasema, "U hali gani?"

Naye akasema—naye akasema, "Vema, ulitaka nini?"

Nikasema, "Mama, ninatoka kwenye Kampuni ya Utumishi wa Umma." Nikasema, "Wao. . . Mimi. . . walinituma kukata umeme huu," nikasema.

129 "Loo," akasema, "unajua, nilisahau yote kuuhusu." Akasema, "Mama aliniambia hivi majuzi nichukue ile bili ya umeme, nawe unajua, nikasahau tu." Wakati huo ilikuwa saa nne naye hakuwa ametoka kitandani.

130 Kwa hiyo nikasema, "Vema, chukua bili, nami nitakupa tu risiti yake, nasi tutauacha, maana kama nikiukata, itakugharimu dola mbili kuuunganisha tena."

"Loo," akasema, "Asante."

Nami nikasema, "Vema."

131 Naye akaanza kuvuka sa—sakafu na alikuwa ameifungua maskini redio hiyo, na huyu hapa Clayton McMichen, ama yeyote yule, namna fulani ya mmoja wa wahuni hawa hapa wa *Georgia*, mapaka-dume, *Mapaka-shume*, ama *wowote wale*, alikuwa na namna fulani ya—ya . . . alikuwa akicheza fidla hii ya kale, mwajua, akifanya, akicheza maskini ule wimbo kuhusu "futi tano mbili na kufunikwa na manyoya," na yote namna hiyo, "pitia," na upuuzi huo wote, naye alikuwa akiendelea kucheza namna hiyo.

132 Naye akaanza kuvuka sakafu, naye maskini msichana huyo alikuwa amepagawa sana na roho ya namna hiyo, akafanya, "*Tuutleli*, *tuutleli*, *tuutleli*," kote sakafuni. Sasa, sisemi hayo kimzaha, ni—ninawaambia yaliyo kweli. Naye akazunguka-zunguka akipiga makelele, "*Tuutleli*, *tuutleli*, *tuutleli*, *tuutleli*," naye akasahau nilikuwa nimesimama mlangoni.

133 Ndipo basi wakati mtu huyu wa dansi, mwajua, aliyekuwa na fidla, akasema, "Sasa, ninyi nyote njoni kwenye maskini *Greenbrier Ridge* usiku wa leo, tutakuwa huko nje, nasi tutacheza roki," ama chochote kile kilichokuwa, akashuka, akamtupia busu, akasema, "Kwaheri, maskini kipenzi," kasema, "Nitakuwa papo hapo!"

Nilisimama tu na kungoja, ndipo nikawazia, "Maskini mtoto." Mnaona? Ni aibu, msichana mdogo, mrembo.

134 Nikangojea kidogo, naye akasema, "Loo, samahani," akasema, akaja na pesa, mwajua, akasema, "Ninapenda tu kucheza *donsi* vizuri sana." Kujionyesha kwa mapambo, sasa, mwajua, si *donsi*. Kwa hiyo akasema . . . D-a-n-s-i haiandikwi *donsi*. Kwa hiyo akasema, "Ninapenda sana kucheza *donsi*." Akasema, "Unajua nini?" Akasema, "Mimi hupoteza tu . . . "

Nikasema, "Niliona hilo." Na kwa hiyo, nikapokea tu deni yake, nikasema, "Asante sana," kisha nikaondoka.

135 Baada ya kitambo kidogo, nilitoka nikachukua maagizo zaidi kisha nikaja. Nami nilikuwa na mahali pale ambapo mtu fulani alikuwa amepanda na kusukuma nyaya kwenye mita, na kuutumia tu bila hiyo, huku mtu fulani mle ndani akipiga pasi. Mbona, kama walikuwa wameikatia waya hapo, elfu mbili

mia tatu zingalipitia hapo, ingemwua mwanamke ameshika pasi mkononi mwake.

136 Kwa hiyo ilinibidi kupanda juu na kukata ncha hizo, kusudi wasiweze kuziuganisha moja kwa moja namna *hiyo*. Kwa hiyo, nikaukata tu namna *hiyo*, nikashuka, naye Daktari Brown alikuwa akishuka kuja mtaani. Akasema, "Halo, Billy!"

Nami nikasema, "Halo hapo, Dk. Brown." Jamani, yeye ni mtu mzuri sana, mhubiri wa Kimethodisti.

Naye akasema, "U hali gani asubuhi ya leo?"

Nikasema, "Salama, salama."

Akasema, "Ninyi Wabaptisti kweli mna wakati mzuri huko juu, sivyo?"

Nikasema, "Loo, naam, bwana. Tunaninii tu. . . "

Akasema, "Unapataje umati huo ulio nao kule kila Jumapili usiku, Billy?"

Nikasema, "Ninawapa vidonge."

Naye akasema, "Vidonge vya aina gani?"

Nikasema, "Vidonge-*injili*." Uh-huh.

Naye akasema, na kwa hiyo, "Loo," akasema, "hujapoteza lolote la wazo lako la kusini."

Nikasema, "La, la, hiyo ni kweli."

137 Akasema, "Unajua nini, Billy?" Akasema, "Hivi majuzi. . . Nina wafuasi mia tano kwa kanisa lile kule chini," naye akasema, "Nimetuma kadi mia tano kuwafanya watu hao waahidi kwamba wangekuja miezi sita kwa mwaka kwenye shule ya Jumapili. Katika mwaka wangejiandikisha mara sita katika—katika. . . wangejiandikisha angalau miezi sita katika mwaka, watakuja." Kisha kasema, "Unajua ni wangapi waliojibu?"

138 Nami nikasema, "Sina habari, Ndugu Brown." Sasa, alikuwa ni mtu mzuri, naam, bwana, ninaamini mtu halisi, wa kweli. Nami nikasema. . . Siamini alikuwa na Roho Mtakatifu, la, bwana, siamini. Lakini ninamaanisha, ninaamini yale yeye—yale yeye aliyohubiri aliyaamini, naye alikuwa mkweli kufikia hapo.

139 Kama vile yule mtu mweusi, akila tikiti maji, alisema, akala kipande chake, na kusema, "Vipi kuhusu hilo, Mose?"

140 Akasema, "Hilo lilikuwa ni tamu, lakini kuna la *zaidi*." Na hivyo karibu ndivyo ilivyo, mnaona. Kwa hiyo sehemu hiyo ilikuwa sawa kabisa kadiri alivyoenda, bali hakwenda mbali sana.

141 Kwa hiyo basi nikasema, "Ni wangapi waliojibu, Ndugu Brown?"

Akasema, "Wawili walijibu Jumapili iliyopita." Akasema, "Unaonaje hilo?"

Nikasema, “Vema, hiyo ni mbaya sana, Ndugu Brown.”

142 Nikasema, “Unajua nini, Ndugu Brown, ninataka kukwambia jambo fulani dogo, lililotukia muda mfupi uliopita.” Nikasema, “Nilikuwa huko chini New Albany,” nilikuwa Jeffersonville wakati huo, nikasema, “Nilikuwa huko chini New Albany,” maili tatu tu chini, nami nikasema, “Nilikuwa nikimkatia umeme kule mtu ambaye hakulipa bili yao. Nikaenda nikabisha mlango,” ndipo nikamwambia kuhusu yule msichana.

143 Nami nikasema, “Msichana huyo, alikuwa amechukuliwa sana, alienda kote sakafuni, baada ya kuzungumza nami, na muziki huo ulikuwa na ushawishi mkubwa sana kwake, hata akaenda kote sakafuni akiimba, ‘*Tuutleli*, *tuutleli*, *tuutleli*,’ na—na kumtupia busu huyo Clayton McMichen,” ama lolote lililo jina lake kwenye *Greenbrier Patch*, ama popote alipokuwa aende huko nje. Nikasema, “Unafikiri itamlazimu mtu fulani huyo kutia kadi sahihi kumfanya aende huko Jumamosi usiku?”

Akasema, “Vema, la.”

144 Nikasema, “Angeweka rehani zile, hizo nguo chache alizokuwa amevaa, apate kwenda huko.” Hiyo ni kweli. “Kwa nini?” Nikasema, “Kwa sababu ndani yake kulikuwako na roho ya kucheza dansi.” Ndipo nikasema, “Sasa, Ndugu Brown, samahani kwa ujinga wangu, wala usifikiri kwamba ninajaribu kukwambia jambo fulani, lakini nataka kukwambia jambo fulani sasa hivi.” Mnaona? Nikasema, “Ninii . . . Kama hao watu walimpenda Mungu kama huyo mwanamke alivyopenda kucheza dansi, wangekuwa kanisani, isingekubidi kutia sahihi kadi yoyote kuwapeleka kule.”

145 Na hapo ndipo ilipo, ndugu, kanisa limepoteza bidii yake, upendo wake kwa ajili ya Injili, kwa ajili ya nguvu, kwa ajili ya Roho Mtakatifu, limezipoteza. “Je, hapana zeri katika Gileadi, huko hakuna tabibu? Mbona basi haijarejea afya ya binti ya watu wangu?”

146 Inanikumbusha kama m—mtu anayekufa kwenye vipandio vya mlangoni pa daktari wakati daktari anayo tiba ya ugonjwa wake, jambo lile lile. Kweli. Kama mtu ana ugonjwa, na daktari ana dawa ya ugonjwa huo, naye mtu huyo anakuja na kukataa kunywa dawa ya huyo daktari, basi kama huyo mtu akifa papo hapo kwenye vipandio vya mlangoni pa daktari, unaweza kumlaumu daktari? Je, unaweza kuilaumu hiyo dawa? Ni nani wa kulaumiwa? Mwenyewe. Hiyo ni kweli. Huwezi kumlaumu daktari, anayo dawa, yuko tayari kuitoa. Huwezi kuilaumu dawa, sayansi imeibuni kwa ajili ya ugonjwa huo. Kwa hiyo, anakufia papo hapo mlangoni, lakini usimlaumu daktari. Hiyo ni kweli kabisa.

147 Ni jambo lile lile tu siku hizi, watu wanakufia moja kwa moja kwenye marefu ya kanisa kutokana na dhambi. Si kwa sababu

hatuna dawa, si kwa sababu hatuna matabibu, ni kwa sababu watu hawataki kuinywa. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

148 . . . na kuwazia ya kwamba angeweza kuushughulikia mkono wako, ni hatari kutokufanya hivyo, unapaswa kufanya hivyo, ni hatari usipofanya hivyo. Pia kuna wakati hatukuwa na dawa nyingi, watu walikufa kwa dondakoo, bali walipata dawa yake. Polio, dawa ya Salk, hiyo ni—hiyo ni sawa, hakika na—nathamini hiyo. Ninaamini mtu angekuwa mnyenyekevu zaidi . . .

149 Unasema, "Ndugu Branham, unaamini katika uponyaji wa Kiungu?" Huo wote ni uponyaji wa Kiungu, kila sehemu yake ni uponyaji wa Kiungu. "Mimi ndimi Bwana nikuponyaye magonjwa yako yote." Naam. Kila sehemu yake ni uponyaji wa Kiungu. Kama hospitali na ninii, na vitu kama hivyo si ninii . . .

150 Niambieni mahali palipowahi kuwa na daktari mmoja ambaye angeweza kuponya ugonjwa mmoja, ama uniambie mahali walipopata dawa itakayoponya ugonjwa fulani. Nilihojiwa huko kwa Mayo, mliyaona katika *Reader's Digest*, na kadhalika, Donny Morton, aliponywa hapa juu, wakaniita, ndipo wakasema, "Hatudai kuwa waponyaji, Bw. Branham, tunadai tu kusaidia maumbile, kuna Mponyaji mmoja, huyo ni Mungu." Hakika.

151 Nilikuwa nikihubiri juu ya jambo hilo wakati mmoja, mtu fulani akasema, "Vipi kuhusu penisilini, Ndugu Branham, halafu kwa ninii—kwa ajili ya, ma—mafua makali?"

152 Nikasema, "Vema, ni kama tu vile nyumba yako imejaa panya, nawe utie sumu, kuwaua panya, hilo halizibi hayo mashimo." Nikasema, "Penisilini huua tu vijidudu, haininii . . . haijengi tena seli za damu, na kadhalika." Mungu ndiye Muumba pekee anayeweza kuumba chembechembe za damu, na—na kalisi, na kwa hiyo, daktari huurudisha mkono, hauponyi.

153 Vipi kama nikipiga gari langu hendeli, na kuvunja mkono wangu, nikaingia ndani, kasema, "Daktari, uponye mkono wangu upesi sana, nitamaliza kupiga gari langu hendeli." Mnaona? Hawezi kuuponya, yeye huuweka tu pamoja wakati Mungu anauponya . . . ? . . . Yeye anayasaidia tu maumbile, Mungu ndiye Mponyaji. Kwa hiyo, kuna ninii tu . . . Kuna tiba, na hiyo ni nzuri, na kama hutumii tiba hizo, basi ni hatari.

Vema, unasema, "Hivi unaamini katika uponyaji wa Kiungu, na kuami- . . . ?"

154 Vema, sikiliza ndugu, daima ninaomba kila mchana na usiku wapate kugundua kitu fulani kwa ajili ya kansa. Waangalieni maskini hao watu. Chochote . . . Hakuna kitu chema kingeweza kuja, isipokuwa kitoke kwa Mungu. Hiyo ni kweli. Tungefanya nini leo kama hatungekuwa na sehemu hizo?

155 Ninajua nilipoanza kwa mara ya kwanza miongoni mwa Wapentekoste, wao—wao, wengine walitetemeka nyuma ya

mlango ulio nyuma yangu. Lakini mnaona yale Mungu aliyofanya, Yeye alisonga tu mbele moja kwa moja, Yeye anawapenda, na kuwaacha tu waendelee, kwa vyovyote vile. Yeye huponya vivyo hivyo tu, kwa hiyo haileti tofauti yoyote. Naam, hakika, uponyaji wote ni wa Mungu, "Mimi ndimi Bwana akuponyaye magonjwa yako yote."

156 Nimesema hilo mara nyingi: Vipi kama nikikata mkono wangu hapa? Hawana dawa ulimwenguni ingeweza kuponya jeraha hilo la kisu, hata moja. Kama ingeponya jeraha la kisu hapo, ingeponya jeraha la kisu kwenye koti langu, ama kwenye dawati hili.

157 Unasema, "Haikutengenezewa koti lako wala dawati, ilitengenezwa kwa ajili ya mkono wako."

158 Vema. Nina jeraha la kisu mkononi mwangu na nikaanguka nikafa. Wananipeleka kwenye chumba cha maiti, na kuupaka mwili wangu dawa inayonifanya nionekane wa kawaida kwa miaka hamsini. Wanindunge sindano ya penisilini kila siku, wanitie Methioleti, na Mercurokromu, waushone madaktari watoke Ujerumani, nao wanioshe kwa mvuke, na chochote zaidi wanachotaka kufanya. Jeraha hilo litakuwa tu kama lilivyokuwa wakati lilipokatwa miaka hamsini iliyopita. Sasa, kama dawa inauponya mwili wa mwanadamu kwa nini isiuponye?

"Vema," unasema, "hauna uhai wowote."

159 Basi dawa si mponyaji, uhai ndio mponyaji, mnaona. Basi niambieni uhai ni nini, nitawaambia Mungu ni Nani. Mungu ni uhai, kweli kabisa.

160 Sasa, dawa, *zaidi sana*, ni hatari kuinywa. Lakini, loo, huenda ukaepuka kwa kutokunywa dawa ya daktari, bali huwezi kuendelea bila Dawa ya Mungu, zeri Yake. Huwezi kufanya hivyo. Ita—hiyo . . . Hakika huwezi kufanya hivyo.

161 Halafu basi, wanapataje dawa? Vema, *sayansi* fulani inasomea vitu vingi sana kisha wanavichemsha pamoja, na kuviweka kwenye neli ya majaribio, na kadhalika, na kuvichemsha. Baada ya kitambo kidogo wanapofikiri wameipata, wanadunga nayo nungubandia, na kama akinusurika nayo, basi wanakudunga wewe nayo. Sawa.

162 Nanyi mwajua, dawa itaua watu fulani, na kuwasaidia wengine. Penisilini imeua watu wengi kadiri ya wale imesaidia, karibu hivyo. Hiyo ni kweli. Nilikuwa nikisoma hivi majuzi ambapo mwuguzi mmoja amekunywa penisilini kwa miaka kumi na mitano iliyopita, au zaidi, ndipo akanywa dozi moja nayo ikamwua, mara moja. Mnaona? Sasa, mnaona, itaua wengine na itasaidia wengine, kwa sababu watu wote hawajaumbwa kama nungubandia. Kwa hiyo, tunaona ya kwamba—ya kwamba—hiyo ndiyo sababu husaidia wengine na—na—na kumwua mwingine. Hiyo ni kweli. Lakini dawa ya Mungu huwasaidia wote. Ni tiba, si dawa, ni tiba. Amina. Sawa.

163 Wanasema mwuaji namba moja ni ugonjwa wa moyo, uh-uh, si—sikubaliani nawe, mwuaji namba moja ni shida ya dhambi, kutokuamini, huyo ndiye mwuaji namba moja. Loo, naam.

164 Unajua, watu husema, “Siwezi kuacha kuvuta sigara, kamwe siwezi kuacha.”

Mwanamume akisema, “Nimekuwa si mwaminifu kwa mke wangu, Ndugu Branham, bali kamwe siwezi kuacha, mwanamke mmoja hanitoshi.”

165 Na huyo mwingine, mwanamke mmoja alisema, “Loo, sijui Ndugu Branham, nilianza tu nilipokuwa msichana mdogo, kuzurura, kamwe siwezi kuacha. Hii inavunja nyumba yangu. Mimi . . . ”

166 Mnajua nini? Ni kwa sababu tu hukuijaribu sumu hiyo, hivyo tu. Unakataa tu kuinywa. Tuna vitu vinavyoua hivyo. Tuna vitu vinavyokufanya uishi kwa ustahifu kwa mke wako. Amina. Tuna kitu kinachokuondolea tamaa ya sigara. Tuna kitu kinachokuondolea dhambi, lakini unakataa kukichukua, hivyo tu. Kamwe hutaijaribu hiyo dawa, unahofia hadhi yako ya kijamii, unaogopa huko kuzaliwa upya.

167 Mnajua, kuzaliwa upya ndiko watu wanataka kukwepa, wanataka kukwepa hiyo hoja, kwa hiyo ibilisi anaikarabati, kasema, “Unapoamini, hapo ndipo unapozaliwa mara ya pili.” Hiyo si kweli.

168 Sikilizeni, kuzaliwa kwokwote, kama nilivyosema hapo awali, kuzaliwa kwokwote ni mchafuko. Sijali kuko wapi. Kama kuko kwenye zizi la nguruwe, ni mchafuko, mchafuko wa nguruwe wakizaliwa huko nje, ni jambo la kuchukiza sana. Kama kulifanyika huko nje kondeni wakati ndama anapozaliwa, ni jambo la kuchukiza sana, mchafuko mbaya. Kama ni huko nje kwenye chumba cha hospitali kilichopambwa waridi, bado ni mchafuko. Nako kuzaliwa upya ni mchafuko, bali huna budi kuwa na kitu hicho chenye mchafuko ili kuleta Uzima mpya. Amina.

169 Hiyo ndiyo shida ya watu siku hizi, wanahofia kutaosha baadhi ya rangi usoni mwao ama kuwafanya wanyoke, wanayo dawa, bali hawataki kuinywa. Naye Mungu atakuuliza, “Kwa nini,” siku moja, “hukufanya hivyo? Kwa nini hukufanya?”

170 Kuna dawa, kuna zeri katika Gileadi, huko kuna matabibu. Lakini sababu yake ni kwamba watu hawataki kumkubali huyu Tabibu, wanataka aspirini badala yake, hawataki kuubaini huo ugonjwa.

171 Unapoingia kwa daktari na kumwambia, “Mimi—mimi ni mgonjwa, tumbo langu linauma, kichwa changu kinauma,” akitaka kukuondosha, vema, jambo la kwanza atakalofanya, atakupa fomula ndogo iliyo na aspirini ndani yake, na kukuondosha. Huyo si daktari, anajaribu kukuondosha. Daktari

halisi atauchunguza ugonjwa huo mpaka apate sababu yake, ndipo aanze kufanya kazi kutoka hapo.

172 Ndiyo sababu tunapata kasoro nyingi kutoka kwenye ibada hizi, *zinazoitwa* ibada za uponyaji. Unashuka kule na uko mstarini, unaangalia huo upambanuzi, unashuka na kutafuta kitu hicho, mpaka unapata chanzo chake. Unapopata chanzo chake: "Jambo ndilo hili: unafanya *hivi*, unafanya *vile*," maisha machafu na kadhalika, watu wakija jukwaani.

173 Mmeliona katika mikutano, sivyo? Inueni mikono yenu kama mmemwona Roho Mtakatifu akitambua mambo hayo na kufichua hizo dhambi, wanaume wasio waaminifu kwa wake zao, na mambo kama hayo. Je, limewahi kushindwa? Daima ni kweli. Inakupasa. . .Ungeweza kumwaga mafuta kichwani mwao, na kukanyaga kwa kishindo, na kupiga mayowe, na kushikwa na mitetemeko na mizizimo, na kadhalika, ibilisi huyo atakaa papo hapo, kwa sababu ana haki ya kukaa hapo, mpaka utakapoikiri dhambi hiyo, na kuisahihisha, na kumwacha Roho Mtakatifu aingie. Haleluya! Kurudi kwenye Pentekoste!

174 "Je, hapana zeri katika Gileadi? Huko hakuna tabibu?" Hakika, wapo, lakini watu hawataki hiyo dawa, hawataki dawa ya Mungu, hivyo tu. Loo, naam, kuna—kuna—kuna zeri katika Gileadi, na huko kuna Tabibu, bali watu hawataki kumsikiliza Tabibu, um-hum, wanaogopa kuzaliwa upya.

175 Kulikuwa na wakati ambapo da—dawa, hata kwa dhambi, haikuwa imenyoka sana, kwa sababu ilikuwa ya wana-kondoo, na hua, na ng'ombe, na kadhalika, lakini ni bora zaidi sasa, imekuwa na tofauti fulani.

176 Mnajua, kama nilivyosema, wakati madaktari wanapotaka kujaribu dawa yao, wanamdunga nungubandia na kuona jinsi anavyotenda. Lakini mnajua, wakati Mungu alipoishusha dawa Yake, hakumdunga nungubandia, alimdunga Mwanawe, Mwenyewe. Yeye alijifanyia Mwenyewe mwili, mnaamini hilo? Yeye alimtia uvuli bikira Mariamu na kujiumbia Mwenyewe mwili, akabadilisha kinyago Chake kutoka kwa Mungu Yehova, akawa Mtu hapa duniani kujidhihirisha Mwenyewe kupitia mwili. Wala Yeye hakuipa nungubandia!

177 Nami ninataka kunyosha baadhi ya fundisho hili la kijamii hapa ambalo wanasema kwamba Yeye alikuwa tu ni nabii. Kamwe hakumpa nabii, alijipa Mwenyewe. Daktari yeyote mzuri atajaribu dawa yake mwenyewe, aone kama inafaa. Yesu alijipa Mwenyewe.

178 Alibatizwa Yordani kwa Roho Mtakatifu. Yohana alishuhudia, akimwona Roho wa Mungu kama hua akishuka juu Yake, Sauti ikisema, "Huyu ni Mwanangu mpendwa, ninayependezwa kukaa ndani Yake."

179 Waliiangalia: Alipojaribiwa, hiyo dawa ilishikilia; alipopigwa usoni, ilishikilia; alipotukanwa, hakujibu;

walipomfunga kitambaa kichwani Mwake na kumpiga kichwani kwa fimbo, kasema, “Kama wewe ni nabii, sasa tuambie ni nani aliyekupiga,” hiyo dawa ilishikilia; walipomng’oa ndevu usoni Mwake na kumtemea mate usoni Mwake, nao askari walevi wakamcharaza na kumtemea mate usoni Mwake, na kumng’oa makonzi ya ndevu, ilishikilia; pale Kalvari, ilishikilia, haleluya; katika saa ya kufa ilishikilia; alipokufa ilishikilia; wakati Nafsi Yake iliposhuka kuzimuni, ilishikilia.

180 Lakini kwenye asubuhi ya Pasaka ilithibitika ilikuwa ni Mungu. Dawa anayotoa ni Uzima wa Milele. Unawezaje kuiweka kuzimuni? Unawezaje kuiweka mahali pengine popote? Malango ya kuzimu, mauti, na kaburi yasingeweza kuishikilia. Alifufuka tena siku ya tatu, akathibitisha kwamba hiyo dawa ilikuwa halisi. Amina. Akafufuka! Loo, walipomwona akifufuka! Wale manabii walikufa na kuzikwa, lakini Yesu alifufuka tena.

181 Dawa ya Mungu ilikuwa imeshuka kama hua kutoka juu, ikamulika juu ya Mwanawe Mwenyewe, Naye akaishi maisha, ya amani, alienda huku na huko, sio akiwa wa kujitangaza, mtu mkubwa mwenye kiburi, aliyejaa majivuno, “Mnaona ninachoweza kufanya?” Alijificha, na kujizuia, kisha akarudi kutoka kwa watu, na kadhalika, aliitwa kila kitu ambacho angeweza kuitwa, Naye akawahudumia moja kwa moja walio wanyenyekevu, wagonjwa, makahaba, na kila kitu kilichokuwako, ilishikilia, kila jaribio lilishikilia, na katika mauti ilishikilia.

182 Maishani ilishikilia, katika mauti ilishikilia, na ikathibitisha katika ufufuo kwamba ilikuwa ni Uzima wa Milele. Huo ni Uzima wa Mungu Mwenyewe. Neno *Milele* linatokana na neno la Kiyunani la *Zoe*, ambalo linamaanisha “Uzima wa Mungu Mwenyewe uko ndani Yake.” Na unapompokea Roho Mtakatifu, ni Uzima wa Milele, na Uzima wa Mungu Mwenyewe uko ndani yako, huwezi kufa zaidi ya vile Mungu awezavyo.

183 Alijigawa Mwenyewe, wakati aliposhuka kwenye Siku ya Pentekoste na kujigawa Mwenyewe, Ndimi za Moto, ile Nguzo ya Moto, ilitawanyika kote kanisani na kukaa juu ya kila mmoja wao, Mungu akijigawa Mwenyewe miongoni mwa Kanisa Lake. Utukufu! “Siku hiyo mtajua ya kwamba Mimi niko ndani ya Baba, Baba ndani Yangu, na Mimi ndani yenu.” Amina. Hiyo ni Pentekoste, hiyo ndiyo baraka halisi.

184 Hiyo dawa ilishikilia, naam. Na ni nini kilichotukia? Baada ya hayo, hao wote waliona ya kwamba Huyo alikuwa ni Yesu yeye yule. Tomaso akasema, “Sina budi kuweka mkono wangu mkononi Mwake, na ubavuni Mwake.” Halafu basi akasema, “Mungu wangu! Bwana wangu na Mungu wangu!” Hao wengine wanaiona hiyo, waliiamini.

Akasema, “Je, mngetaka kuwa jamaa waliochanjwa?”

Kasema, "Naam, ninataka baadhi ya chanjo hiyo, pia, maana ninataka kufufuka, pia, katika siku ya mwisho."

185 Kasema, "Nitawaambia mtakalofanya: Nendeni kwenye mji wa Yerusalemu, na mwache mahubiri yenu, mwache uimbaji wenu, mwache kushuhudia kwenu, lakini nendeni kule kwenye mji wa Yerusalemu mkangoje, kwa kuwa nitashusha lundo lake kutoka Mbinguni."

186 Basi alipokuja, hakuwa ni m—mhubiri akisema, "Sasa, simameni, halafu tutakuja madhabahuni, na kunyunyizia mkung'uto mdogo wa chumvi, na kadhalika." Ama kasisi kupanda aje barabarani huku ukosi wake umepinduliwa, aseme, "Toa ulimi wako, tutakula ekaristi takatifu," na yeye akinywa divai. Walibadilisha mambo hayo yote, hayo ni mafundisho ya mwanadamu.

187 Lakini alipoituma hiyo dawa kule chini, kwa ghafla, sauti ikatoka Mbinguni, kama upepo wenye nguvu ukienda kasi, nayo ikajaza nyumba yote walimokuwa wameketi. Ndipo Mungu akawachanja watu mia na ishirini, dawa ikaingia ndani yao, Uzima wa Milele. Kundi la waoga, hawakuwa waoga tena, walipitia kwenye madirisha, milango, na kadhalika, wakaingia mitaani, nao walikuwa wakiyumbayumba.

188 Sikiliza, dada yangu Mkatoliki, bikira Mariamu aliyebarikiwa alikuwa pamoja nao, huku akiwa ni mama wa Bwana wetu Yesu Kristo. Na kama Mungu hangemruhusu kuja Mbinguni, mpaka alipopanda juu na kumpokea Roho Mtakatifu na kutenda kama hao wengine, akayumbayumba kana kwamba alikuwa amelewa, utaendaje Mbinguni ukipungukiwa chochote cha hayo? Wazia hilo.

189 Wewe mwanamke wa Kimethodisti, unayefikiri kwa sababu wewe ni mfuasi wa karamu ya kadi, nanyi Wabaptisti ambao mmebatizwa majini na kuwazia hilo latosha, nanyi Church of, *mnavyojiita*, Church of Christ, nanyi wengine, nanyi Waadventista mlio na siku ya saba, ninyi Wapentekoste mnaojiunga tu na dhehebu mtaendaje Mbinguni na chochote pungufu ya ubatizo wa Roho Mtakatifu? Utakuwaje kama hujachanjwa? Huna budi kuwa na kitu kile kile. Kweli.

190 Naam, wote walikuwa wakiyumbayumba kama walevi. Wa—wao walikuwa wamesimama huko nje, wakiwacheka, wakisema, "Watu hawa wamelewa kwa mvinyo mpya."

191 Hatimaye, kulikuwa na maskini mhubiri mmoja aliyesimama kwenye sanduku la sabuni, ama kisiki, hakuwa na elimu yoyote, asingeweza kuandika jina lake, hakuwa amewahi kuwa katika baadhi ya shule zetu, lakini alisema, "Enyi watu wa Uyahudi, na ninyi mkaao Yerusalemu, lijueni jambo hili: Watu hawa hawakulewa, kama mnavyodhania, kwa maana ni saa tatu ya mchana. Lakini *hili* ni *lile*." Ndugu, kama *hili* si *lile*, nitaliweka tu *hili* mpaka *lile* litakapokuja . . .? . . .

192 Ilikuwaje? Walichomwa moyoni mwao, nao wakasema, "Wanaume na ndugu, tunapataje chanjo? Ingalipo zeri zaidi katika Gileadi? Je, kuna tabibu yeyote huko?"

193 Naam, walikuwa na zeri nyingi sana. Walikuwa na tabibu. Je, ungetaka kujua jina lake lilikuwa ni nani? Walimwita Dk. Simoni Petro. "Naam, tuna tabibu hapa, nawaambia kweli, yeye anazo funguo za Ufalme. Yeye ana tabibu, tuna zeri nyingi sana."

"Tufanye nini?"

194 Ndipo Petro akasimama katikati yao, akawaambia, "Nitawaandikia maagizo ya dawa, nayo yatakuwa kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, na kwa wote walio mbali, na kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie. Yatakuwa ni maagizo ya dawa ya Milele." Naye akasema, "Tubuni, kila mmoja wenu, mkabatizwe katika Jina la Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea Kipawa cha Roho Mtakatifu. Kwa kuwa ahadi hii ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, na kwa wale walio mbali, hata wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie."

195 Maagizo haya ya dawa yatadumu kwa muda gani? Maadamu Mungu anaita, angali ni Roho Mtakatifu yeye yule.

196 Sasa, jambo ni kwamba, kama daktari wako akikuandikia maagizo ya dawa, basi afadhali uyapeleke kwa muuza dawa anayefaa, maana ukimchukua tapeli muuza dawa ambaye hayachunguzi maagizo hayo vizuri, angeweza kumwua mgonjwa. Nafikiri hilo ndilo lililotukia, tuna makanisa mengi mno ya kale, yaliyokufa, ya kawaida, hayatumii hayo maagizo. Hilo linasikika baya sana, bali ni kweli.

197 Sasa, daktari huyo akiubaini ugonjwa huo, anajua tu kile kinachohitajika, *kiasi fulani* cha dawa kuua kijidudu, *kiasi fulani* cha kiuasumu cha kupoza hiyo sumu, kuizuia isikuue. Unaona? Na kama ukiondoa sumu yote kwake, basi itafanya nini? Mgonjwa wako, haitamsaidia hata kidogo. Ukiondoa kiuasumu chote, utamwua mgonjwa wako kwa sumu. Kwa hiyo afadhali uwe na mwuza dawa halisi anayejua kusoma maagizo hayo, kukwambia la kufanya. Usiyaharibu hayo maagizo. Basi kuna shida gani siku hizi, kumekuwako na watu wengi kupita kiasi wanaoyaharibu. Yaache tu jinsi yalivyo, kisha unywe hiyo dawa. Haleluya!

198 Wamethodisti, Wabaptisti, Presbiteri, Katoliki, baridi, Wapentekoste wa kawaida, ninyi wengine, kuna zeri katika Gileadi, na hawa *hapa* matabibu. Haleluya! Kuna nini? Kuna wengi wao ambao watailipua kila dhambi na kila . . .

199 Je, hakuna zeri katika Gileadi? Hakika, ipo. Huko kuna matabibu? Wengi sana, watalifundisha jinsi tu *hilo* lilivyoandikwa mle, sio kuja tu na kuchukua barua yako, na kusema, "Ninaibadilisha kutoka kwa Methodisti kuingia Baptisti." Loo, jamani! Kusimama na kuchukua kidau cha

chumvi, na kukurushia vidau vichache vya chumvi vya maji namna *hiyo*, na kusema, "Yote yamekwisha, Ndugu, nipe mkono wa kuume wa ushirika, na majaribio ya miezi sita." Upuuzi.

200 Petro alisema, "Tubuni, kila mmoja wenu." Tubuni, geukeni. Hiyo ni kweli.

201 "Vema," mnasema, "lakini Ndugu Branham, nilipopeleka barua yangu, niliwauliza hao hivyo kuhusu hili, nililisoma katika Biblia, lakini wao walisema, 'Loo, hilo lilikuwa ni muda mrefu uliopita, hawana hilo tena.'"

202 Daktari alisema nini? Yeye alisema, "Ahadi hii ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, na kwa watu wote walio mbali, hata wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie."

203 "Enendeni ulimwenguni kote, mkaihubiri Injili." Kwa nani? "Kila kiumbe, kila kiumbe." Umbali gani? "Ulimwenguni kote." Haijaufikia bado. Itachukua muda gani? "Ulimwenguni kote." Itakuwaje? "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio, katika Jina Langu watatoa pepo, watasema kwa lugha mpya, kama wakishika nyoka, ama kunywa kitu cha kufisha, hakitawadhuru, wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya."

204 Tuna zeri katika Gileadi, tuna matabibu, lakini watu wanakataa tu kuinywa. Naye Mungu atauliza, "Kwa nini? Kwa nini hukufanya hivyo?" kwenye Siku ya Hukumu.

205 Sasa, tumemwaga dawa juma hili kwa nguvu kadiri nilivyojua kuimwaga, na moja kwa moja kadiri nilivyojua jinsi ya kuileta. Sasa, usipoipokea, basi Mungu atasema, "Kwa nini?" Siku moja hii Biblia itawekwa mimbarani imefungwa, mhubiri atacheza...ataomba ombi lake la mwisho, taa zitazimwa kutoka kwenye tarumbeta ndogo, nalo jua litatua juu ya kilima kwa mara yake ya mwisho, ndipo Mungu atakuuliza utoe sababu.

Wakati wale wanaoukataa Ujumbe
Wataulizwa watoe sababu, vipi basi?

Vipi basi? Vipi basi?
Wakati kile Kitabu kikuu kitakapofunguliwa, vipi basi?
Wakati wale wanaoukataa Ujumbe *huu* usiku wa leo,
Wataulizwa watoe sababu, vipi basi?

206 Mmehudhuria uamsho huu, Mungu amefanya kila kitu kilicho katika hiki Kitabu kwa ajili yenu, akakithibitisha, maadamu tu unaishi...watu wamempokea Roho Mtakatifu, wamejazwa na Roho wa Mungu, vijana kwa wazee; wa—wametubu dhambi zao; wana furaha moyoni mwao; tumeona uponyaji wa Kiungu ukitendeka, watu wenye ugonjwa wa moyo, na magonjwa mbalimbali wakiponywa; tumemwona Malaika wa Mungu akishuka, akipitia humu jengoni kama tu

Yeye alivyosema kabla tu ya Kuja kwa Bwana hakujatimia, akipambanua roho na mambo kama hayo; matamshi ya kinabii yalitolewa; watu wakanena kwa lugha, na kutabiri, na kulithibitisha Neno huku na huko, mliyaona na kuketi. Utachagua gani usiku wa leo, Hollywood ama Mbingu takatifu? Utaulizwa utoe sababu siku moja, vipi basi?

207 Wakati mmoja kulikuwako na mwanamke mkongwe hapa nchini, alikuwa yuafa, alikuwa yuafa kwa njaa, fukara. Kwa hiyo, mtu mmoja akamkabidhi kwa mamlaka, shirika la kutoa misaada. Nao wakamwendea mwanamke huyu, wakamwambia, "Tumekuja kuchunguza kesi yako, nasi tunataka kujua kuna—kuna shida gani." Kasema, "Hivi wewe huna jamaa?"

Akasema, "Nina mwanangu mpendwa."

Kasema, "Wapi . . .?"

Kasema, "Yeye ni mfanyabiashara."

"Yuko wapi?"

"Yuko India."

"Mbona," akasema "ati yeye ni mfanyabiashara?"

Kasema, "Naam."

Kwa hiyo kasema, "Kwa nini asikutumie kitu?" Kasema, "Amekuwa huko kwa muda gani?"

Kasema, "Yapata miaka kumi." Kasema, "Loo, yeye ni mfanyabiashara aliyefanikiwa sana."

Kasema, "Vema, kwa nini hakusaidii?"

208 Kasema, "Kamwe siwezi kumwomba, kamwe siwezi kufanya hivyo, yeye ni mvulana mzuri sana," kasema, "Kamwe siwezi kumwomba jambo hilo." Kisha kasema, "Ninamwandikia barua, naye huniandikia barua nzuri sana ambazo mvulana yeyote angeweza kumwandikia mamake, naye huniambia jinsi anavyonipenda." Lakini kasema, "Lakini kamwe nisingeweza kumwomba jambo hilo."

Basi kasema, "Vema, unapaswa kumwambia."

209 Kasema, "Kamwe siwezi kufanya hivyo, kumwambia mwanangu kwamba mimi ni maskini sana, na kadhalika," kasema, "Nisingeweza kabisa kufanya hivyo." Lakini kasema, "Yeye hunitumia picha nzuri sana nilizowahi kuona maishani mwangu."

Basi kasema, "Vema, ni picha za aina gani?"

Kasema, "Loo, picha nzuri ndogo, karibu ukubwa *huu*, mraba."

Kasema, "Naweza kuona moja?" Kasema, "Umeziweka wapi?"

210 Akasema, “Ninaziweka katika Biblia yangu.” Kwa hiyo maskini huyo mama akavuka sakafu, naye akaichukua Biblia yake, akaanza kuzitoa, akazitoa.

211 Huyo mpelelezi akaziangalia, alikuwa ni mwanamke tajiri. Zilikuwa nini? Zilikuwa ni hati za benki kutoka India, zilikuwa na picha za kupendeza. Alizipata wapi? Katika Biblia yake. Alikuwa tajiri wala hakujua. Alizipata wapi? Katika Biblia yake.

212 Haikubidi kutenda kama walimwengu, si lazima ufungwe kabisa, wewe ni tajiri. Unaupata wapi? Katika Biblia. Uliichunguza yote, ukawazia kilikuwa tu ni kitabu cha picha, ama *Hadithi Ya Kweli* nyingine, bali sivyo, ni Neno la Mungu. Wewe ni tajiri!

Mimi ni mtoto wa Mfalme!
Mimi ni mtoto wa Mfalme!
Pamoja na Yesu Mwokozi wangu,
Mimi ni mtoto wa Mfalme!

Baba yangu ni tajiri wa nyumba na mashamba,
Anashikilia utajiri wa ulimwengu mikononi Mwake!
Wa marijani na almasi, ya fedha na dhahabu,
Makasha Yake yamejaa, Yeye ana utajiri usioelezeka.

Uimbeni.

Mimi ni mtoto wa Mfalme!
Mtoto wa Mfalme!
Pamoja na Yesu Mwokozi wangu,
Mimi ni mtoto wa Mfalme!

213 Na tuinamishe vichwa vyetu. “Je, hapana zeri katika Gileadi? Huko hakuna tabibu? Basi kwa nini Kanisa Langu lingali linatenda jinsi wanavyotenda? Kwa nini Kanisa Langu linaendelea kuniacha? Je, ni kwa sababu hakuna zeri katika Gileadi, kwa sababu hakuna matabibu wa kubaini ugonjwa wao, na kuwafanya wajue kwamba wamekosea?”

214 La, tunao matabibu, tuna zeri, bali watu hawaitaki. Kwanza nilianza kuwakemea wachungaji, lakini nikaja kugundua, haidhuru ninauhubiri jinsi gani, hawasongi, kwa vyovyote vile. Huenda ikawa si mchungaji, huenda ikawa ni kusanyiko. Mnaona? Hiyo ni kweli. Ukitaka, kuna zeri katika Gileadi.

215 Ni wangapi wangetaka kuja kwa Tabibu Mkuu usiku wa leo, dhambi zako zote zipate kuondolewa kwako, upate kuwa na furaha isiyoneneka, na iliyojaa utukufu moyoni mwako? Waweza kuinua mkono wako? Useme, “Niombee, Ndugu Branham.” Mungu akubariki, mama, hapa. Mungu akubariki, ewe kijana. Mungu awabariki huko nyuma. Mungu awabariki huko juu. Hilo ni zuri sana. Loo, hakika. Mungu akubariki hapa, bwana.

216 Huko juu kwenye roshani, je, ungetaka Tabi-. . .Mkuu? Mungu akubariki, naam bwana, ninauona mkono wako mkono wangu wa kulia. Waweza. . .? Na mama huyu hapa, Mungu akubariki, ewe msichana. Uamuzi mzuri sana wa kufanya.

217 "Je, hapana zeri katika Gileadi? Huko hakuna tabibu? Basi kwa nini watu Wangu wangali wamelemewa katika dhambi? Kwa nini wangali wanaenda huku na huku kwa ajili ya mambo ya ulimwengu? Hivi hakuna ridhaa ya kutosha katika Injili Yangu kushughulikia kila shauku waliyo nayo? Kuna furaha ya kutosha wanaponipokea Mimi? Hivi siwapi furaha ya kutosha na upendo, hata ingeondoa upendo wote wa ulimwengu kutoka kwao? Nilisema, mwajua, 'Mkiipenda dunia, ama mambo ya dunia, kumpenda Baba hakumo ndani yenu.' Kuna furaha ya kutosha katika kumtumikia Mungu kuwaondoa kwenye mambo ya ulimwengu? Basi mbona hajapona binti ya watu Wangu kutokana na ugonjwa wao wa dhambi?"

218 Je, kunaweza kuwa na mwingine kabla hatujaomba? Inua mkono wako, useme, "Niombee, Ndugu Branham." Mungu akubariki huko nyuma, mama. Loo, hilo ni zuri sana! Mikono saba ama minane imeinuliwa. Kuna wengine zaidi? Sema, "Niombee, Ndugu Branham, na—nataka zeri ya Gileadi." Kuna zeri katika Gileadi.

219 Je, kunaweza kuwa na mtu mwingine angetaka kuwa. . . kuleta dawa ya Roho Mtakatifu nafsini mwako? Waweza tu kuinua mkono wako? Useme, "Mungu, nichanje usiku wa leo kutokana na mambo ya ulimwengu, na unichanje kutokana na kutokuamini kwangu kwote, ili niweze kuwa na imani ya kusimama kama Mkristo halisi." Inua mkono wako, sivyo? Mungu akubariki, bwana. Mungu akubariki, ewe kijana mwanamume, uliyeketi hapa. Mungu akubariki huko nyuma, rafiki yangu. Mungu akubariki, ndugu. Hapa, hilo ni zuri.

220 "Nichanje, Bwana, kutokana na mambo ya ulimwengu. Nilifikiri nisingeweza kuyaacha, lakini kwa kweli, kamwe sijawahi kunywa dawa Yako bado, ningetaka kuinywa, Baba. Acha tu Roho Mtakatifu aje na kuichanja nafsi yangu kutokana na mahangaiko yote ya ulimwengu. Nikumbuke katika maombi, Ndugu Branham, ninainua mkono wangu, kwa sababu ninaamini." Mungu ambariki msichana huyu, aliyeketi papa hapa. Mungu ambariki huyu hapa. Naam, ndugu kijana, Mungu akubariki, hilo ni zuri. Vema. Papa hapa, naam, Bwana abariki, naam, moja kwa moja huku pembeni, ninao wawili. Naam, Bwana anauona mkono wako.

Hebu tuombe pamoja sasa.

221 Baba wa Mbinguni, kwa urahisi na kwa upendo, tunakuja kwenye Chemchemi iliyojaa Damu, iliyotolewa kwenye mishipa ya Imanueli, ambapo wenye dhambi wanatumbukia chini ya gharika hiyo, na kupoteza madoa yao yote ya hatia. Waliinua

mikono yao, Baba, kwa sababu kwamba—kwamba wanaamini. Nasi tunajua ya kwamba wao ni roho moyoni mwao, ndipo Roho Mtakatifu akawajia, na kusema, "Umekosea, umekosea. Kwa nini usinikubali Mimi usiku wa leo?"

Nao wakasema, "Naam, Bwana," ndipo wakainua mkono wao.

222 Sasa, Wewe ulisema katika Yohana 5:24, "Yeye alisikiaye Neno Langu," na Bwana, kadiri nijuavyo mimi nimelihubiri, "Yeye alisikiaye Neno Langu, na," kiunganishi, "kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna," wakati uliopo, "Uzima wa milele, wala hataingia hukumuni, kwenye Hukumu, bali amepita kutoka mautini kuingia Uzimani." Baba, ni—ninaweka hilo mbele Zako, hilo ni Neno Lako. Wewe ulisema, "Mbingu na nchi zitapita, bali Neno Langu halitapita." Ulisema, "Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu, asipovutwa na Baba Yangu kwanza. Na wote alionipa Baba watakuja Kwangu."

223 Sasa, tunafundishwa katika Biblia, "Wote walioamini waliongezwa kwa Kanisa." Sasa, Baba, katika tendo la imani, ninawaweka watu hawa, walioinua mikono yao, katika Kanisa la Mungu aliye hai kwa maungamo ya imani, kwamba wao ni watoto Wako tangu usiku wa leo na kuendelea. Na sasa, Baba, wamekuja kwenye ofisi ya Daktari, wako ndani ya mlango sasa, nao wanataka kumjia yule Tabibu Mkuu wapate kupewa Roho Mtakatifu, ile Chanjo, Zeri, ambayo itawaepusha na mambo ya ulimwengu.

224 Ulisema, "Baada ya kuamini mlitiwa muhuri na Roho Mtakatifu wa ahadi." Ninaomba, Mungu, ya kwamba watapata Roho huyo Mtakatifu wa ahadi kwa kuwa wamefanyika watoto Wako. Tujalie.

225 Sasa, wakati tumeinamisha vichwa vyetu, Nitamwomba kila mmoja aliyeinua mkono wake asimame tu kwa muda kidogo kwa ajili ya maombi. Kila mtu uliyeinua mikono yako, si—siamini ulifanya hivyo kwa kujifurahisha tu, ninaamini kweli ulimaanisha jambo hilo mbele za Mungu katika mkutano kama huu. Simama, hiyo ni kweli, simama kwa miguu yako. Kila mahali, huko juu kwenye roshani, popote ulipo, simama kwa miguu yako. Hiyo ni sawa. Mungu awabariki. Hilo ni jema. Simameni tu kwa miguu yenu kwa dakika moja tu. Huko nje ukumbini, kama ukisimama tu kwa miguu yako, useme, "Ni—ninafanya maungamo hayo mimi mwenyewe." Kuna wengi waliosimama sasa.

226 Sasa, ndugu za—zangu wapendwa, waliozaliwa karibuni, na dada, na—nawazia juu ya ono nililoona. Siku moja kwenye nchi fulani, laiti ningaliweza tu kutembea huko nje sasa, na kukushika kwa mikono yangu, na kukukumbatia. I—isingewezekana katika maisha haya ya kibinadamu, nisingeweza kufanya hivyo, bali kuvuka tu mpaka, siku

moja nitavuka. Mtafurahi sana, nitafurahi sana nitakapowaona, nanyi mnione, nasi tu—tutakuwa ndugu na dada halisi wakati huo. Tuna mguso wake mdogo tu sasa.

227 Sasa sikilizeni, nitawaambia yale Mungu aliyosema, Mungu alisema, "Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu, asipovutwa na Baba Yangu kwanza. Na wote alionipa Baba watakuja Kwangu." Sasa, umekuja kwa sababu unajua hustahili kuja, bali umekuja kwa sababu kitu fulani moyoni mwako kilikwambia ya kwamba umekosea, wala hutaki kukosea tena. Hayo ni maungamo ya kweli. Sasa, Biblia ilisema hivi: "Yeye atakayenikiri mbele ya watu, huyo nitamkiri mbele za Baba Yangu na Malaika watakatifu."

228 Sasa, enyi makasisi, hivyo ndivyo Yesu alivyosema? Alisema hivyo. Sasa, umefanya nini? Umesimama hapa mbele ya angalau watu wasiopungua mia sita, ama labda zaidi, katika jengo hili usiku wa leo, kutoa ushuhuda, "Nimekosea, nami ninamkubali Yesu Kristo kama Mwokozi wangu. Mimi. . .Kuna kitu Fulani kilichonena na moyo wangu, na kusema, 'Huu ni usiku wako,' kwa hiyo ninasimama kwa sababu ninatoa ushahidi kwamba nimekosea; ninataka kusimama hapa niwe shahidi wa Kristo."

229 Sasa, Kristo atakushuhudia. Naye alisema, "Nitawashuhudia mbele za Baba, na Malaika watakatifu."

230 Sasa, wakati mnaposimama jinsi mlivyo, ninawatakeni, kila mmoja, kama mnaamini ya kwamba Yesu ni Mwana wa Mungu, na pale Kalvari wakati hayo mawingu meusi yalipokuwa yakielea juu ya msalaba, radi ilikuwa ikimulika, Yesu akifa, akiona kiu, akilia, Mungu alikuwa akimwaga ghadhabu Yake kali juu ya Yesu, Naye aliichukua mahali pako (Je, unaamini kabisa kwamba hiyo ni kweli, kwamba Yeye aliichukua mahali pako?), nawe sasa utaukubali msamaha Wake, si jinsi unavyojisikia, bali kile unachoamini, kwamba—kwamba Yeye alifanya hivyo kwa ajili yako, kama utaukubali, na kusema, "Bwana, ninii. . .Siwezi kufanya jambo lolote, mimi—mimi ni mwenye dhambi mbaya sana, bali ninakubali msamaha Wako kwa ajili yangu. Ni—ninakubali ya kwamba Wewe ulikufa mahali pangu, ninaamini hilo kwa moyo wangu wote," inua mkono wako, wewe ambaye. . .Naam, hilo ni zuri. Kila mmoja, kila mmoja.

231 Sasa, kadiri nijuavyo katika Maandiko, hayo ndiyo yote yanipasayo kufuata, umeokolewa na. . .hutaingia Hukumuni kamwe, bali umepita kutoka mautini kuingia Uzimani.

232 Sasa, ninawatakeni ninyi Wakristo mliosimama karibu na watu hawa waliosimama, ninataka uinue kichwa chako na kuangalia, ninataka uwape mikono na kusema, "Mungu akubariki, ndugu yangu, dada. Karibu katika Ufalme wa Mungu." Geuka tu, wapeni mikono. Hiyo ni kweli. "Karibu, ndugu yangu Mkristo, dada." Hiyo ni kweli. Ninawaona

wanawake wakikumbatiana, na kadhalika, ajabu sana. "Karibu katika Ufalme wa Mungu."

233 Ninawatakeni sasa mpate kanisa zuri la Full Gospel, acheni mtu fulani awabatize katika ubatizo wa Kikristo, kisha muutafute ubatizo wa Roho Mtakatifu. Sasa, hiyo inakuchanja kutoka kwenye kitu kile kile kilichokuhukumu usiku wa leo, unapita tu juu yake. Unaona, chanjo hukukinga na ugonjwa huo. Chanjo ya Roho Mtakatifu hukupa nguvu za kushinda majaribu yote ya ulimwengu. Hiyo ni kweli, makasisi? Ni ninii yako... ni zeri, ni zeri ya chanjo ambayo...Mnasema, "Ni—nilimjaribu Ndugu Branham, lakini—lakini nikashindwa." Lakini unaona, si kile unachofanya, ni kile Yeye alichokufanyia. Si kile ulicho, ni kile Yeye alicho. Mwamini Yeye.

234 Sasa, hebu...njoni tu Kwake, mtumaini kama Tabibu wako, na umruhusu akuchanje sasa kutokana na majaribu ya... Sasa, utajaribiwa, bila shaka, lakini mmea mzuri, wenye nguvu sio lazima unyunyiziwe, ni imara na una nguvu, upinzani wake huwatupilia mbali vimelea viovu. Na hivyo ndivyo alivyo Mkristo mzuri mwenye nguvu, anaweza kushinda majaribu yote, kwa sababu huyapindua mambo yote ya ulimwengu.

Mwanamke anaweza kusema, "Njoo, mpenzi, hutakuwa wa mtindo wa kale sasa, unaenda kwenye dansi."

"Nilipata Lulu ya thamani kubwa."

"Sasa, unajua utavuta sigara tena."

"La, bwana, nimepata *Kitu* kikubwa zaidi. Loo, ni kikubwa zaidi!"

235 Mungu awabariki sasa. Mnaweza kuketi. Na Mungu awe pamoja nanyi. Ninaomba ya kwamba baada ya mstari wa maombi, kwamba mtakuja kwenye madhabahu ya Mungu, na mtajaza...kujazwa na Roho Mtakatifu usiku wa leo. Ninaomba ya kwamba Mungu Baba yetu atawajalia hilo. Hmm! Yeye si ni wa ajabu?

236 Sasa, tunapofanya hivyo, Roho Mtakatifu mkuu yuko hapa...Nilipokuwa nikiliangalia kusanyiko, ningeweza tu... Ninajua tu tutakuwa na mkutano mkubwa wa maombi kwa ajili ya wagonjwa. Kabla hatujafanya hivyo, hebu na tuwe tu na... Ni wangapi wasio na kadi ya maombi? Sitaki mtu yeyote aliye na kadi ya maombi, maana nitawaombea hapa. Wasio na kadi za maombi ambao ni wagonjwa, inueni mikono yenu. Vema. Sasa, ushikilie tu mkono wako, ili niweze kuangalia huku na huku, inueni mikono yenu katika sehemu hii.

237 Huyu hapa mama, yupo papa hapa, unaweka mkono wako chini sasa. Naam. Huna kadi yoyote ya maombi? Vema, ili kwamba hao watoto wachanga waliozaliwa upya wajue ya kwamba Roho huyu ambaye amekuwa akihubiri hakuwa ni mimi, ilikuwa ni Yeye. Unaona? Kuwafanya wajue...Sasa,

ninawatakeni mniangalie, na kuniamini kama mtumishi Wake. Je, mnafanya hivyo? Je, Yesu angeweza kuliangalia ku—kusanyiko . . . na—na kuamini kwa moyo wao wote ya kwamba Mungu angeweza kuwaponya wagonjwa? Unaamini hilo? Vema, vipi kama ningekwambia kwamba shida yako imekwisha? Ugonjwa wako wa figo, ugonjwa wa kibofu nyongo, na kadhalika, tayari umekuacha, nawe umepona. Sasa, inua mkono wako kama hiyo ni kweli. Vema, sasa nenda tu, na uamini, na uwe na imani, upate afya.

"Kama unaweza kuamini!" Unaamini kwa moyo wako wote sasa?

238 Vema, upande huu. Kuna mwanamke mweusi aliyeinua mkono wake. Unawazia nini, Dada? Je, unaniamini mimi kuwa ni nabii wa Mungu, ama, mtumishi Wake? Nafikiri nina kibali cha kutosha kwenye hili kundi kusema *nabii*. Vema. Unaniamini mimi kuwa ni nabii Wake? Wewe ni mwanamke wa Kushi, mimi ni Mwanglo-Sakson, kama vile Yesu alivyokutana na yule mwanamke kisimani, akazungumza naye kwa dakika moja tu. Sasa, kama Yesu atanijulisha shida yako, utaamini Roho yule yule aliyekuwa juu Yake, Ndiye yuko juu yangu? Utaamini? Basi shinikizo lako la juu la damu litakuacha.

Unaamini? Kuwa na imani, usiwe na shaka, amini tu kwa moyo wako wote. Amini, wala usiwe na shaka.

239 Sasa ninageuza mgongo wangu, ninyi ombeni. Mama fulani anatokea mbele yangu, ameketi upande huu. Anaugua ugonjwa wa basa. Simama. Jina lake ni Bibi Hart. Simama. Je, una kadi ya maombi? La, huna; huihitaji. Uligusa *Kitu fulani*, sivyo?

240 Unaamini kwa moyo wako wote? Sasa, ni wangapi wanaojua ya kwamba Yesu Kristo alisema Roho yuyo huyo angekuwa hapa? Ni wangapi wanaojua ya kwamba hiyo ilikuwa ndiyo ishara ya Masihi wakati Yesu alipokuwa duniani? Ni wangapi wanaojua Yeye aliliahidi hilo kwa Kanisa teule katika siku za mwisho? Vema, hili hapa.

241 Sasa, mnaona, waongofu wapya, baada ya miaka elfu mbili, halijawahi kutukia katika miaka elfu mbili, kwa sababu Nuru za jioni zinaangaza. Biblia ilisema siku itakuja ambayo haitakuwa mchana wala usiku, bali wakati wa jioni itakuwa nuru. Um-hum. Huyo hapo. Sasa, ingekuwa ni Nuru ya namna gani? Jua lile lile lililochomoza mashariki linatua magharibi. Hiyo ni kweli? Nuru ya jioni imekuja. Mnaamini hilo?

242 Sasa, ni wangapi walio na kadi ya maombi? Hebu tuone mikono yenu. Loo, ni, nakisia, karibu mia moja. Sasa, mwanangu yuko wapi? Uligawa kadi zipi za maombi? C, kuanzia moja hadi, hadi hamsini, kuanzia moja hadi hamsini. Ni nani walio na kadi ya maombi namba moja, mbili, tatu, nne, tano? Hebu wasimame kwanza papa hapa. Moja, mbili. Wasemaje? Moja, mbili, tatu, nne, tano, ninawaona. Sita, saba, nane, tisa, kumi, hebu waje.

Pangeni mstari papa *hapa*, huyo mvulana atawapanga mstarini, njoni tu kulingana na namba yako. Kumi.

243 Itakuwa vigumu kujitikisa kutoka kwa upako huo sasa. Hmm! Umekwisha kuanza, unaendelea kusogea juu ya kusanyiko.

244 Kumi na moja, kumi na mbili, kumi na tatu, kumi na nne, kumi na tano, kumi na sita, kumi na saba, kumi na nane, kumi na tisa, ishirini, ishirini na moja, ishirini na mbili, ishirini na tatu, ishirini na nne, ishirini na tano.

245 Njoni tu ninavyowaita, tafadhalini. Njoni moja kwa moja upande *huu*, kisha mrudi moja kwa moja mstarini kule. Ishirini na tano, ishirini na sita, ishirini na saba, ishirini na nane, ishirini na tisa, thelathini, thelathini na moja, thelathini na mbili, thelathini na tatu.

246 Vipi kuhusu ninyi nyote kuingia mstarini papa hapa kuanzia thelathini na tatu papa hapa? Na ndipo wangeweza kuingia kwenye mstari huo huko nyuma. Thelathini na tatu, thelathini na nne, thelathini na tano, thelathini na sita, thelathini na saba, thelathini na nane, thelathini na tisa, arobaini. Papa hapa tu, wakati mwisho wa mstari huo utakapokuja, wanaweza kuingilia moja kwa moja. Arobaini na moja, -mbili, -tatu, -nne, -tano, -sita, -saba, -nane, -tisa, hamsini. (*Amini Tu.*)

Amini tu,
Mambo yote yanawezekana, ninii tu . . .

247 Kama yeyote wa Wafanyabiashara wa Full Gospel yupo hapa, ningetaka kuwa na baadhi ya vitabu hivyo pamoja na hivyo—hivyo, Ndugu Tommy Hicks, kama uko hapa, uliandika sehemu nzuri ya hilo, hiyo ni nzuri sana. Kuna mengi zaidi kidogo tu kwake, bali uliifanya vizuri sana, ninaithamini. Ningetaka kuwachukulia marafiki zangu baadhi yake, nitavinunua, labda mia tatu, ama mia nne, mia tano.

248 Sasa, badala ya kusema . . . Sasa, hebu na tuimbe, "Sasa naamini." Unaamini sasa? Mwajua, Yesu moja kwa moja mwishoni mwa . . . moja kwa moja mwishoni mwa huduma Yake, Wanafunzi Wake wasingeweza kumwelewa, hakuna mtu aliyemwelewa. Mnajua . . . ? Jinsi ambavyo . . . Ni wangapi wanajua ya kwamba wasingeweza kumwelewa? Hakika. Kwa nini? Walidhani Yeye alikuwa na nafsi mbili. La, wakati mwingine ilikuwa ni Yesu akizungumza, wakati mwingine ilikuwa ni Baba ndani Yake akinena. Mnaona? Mnaona? Ilikuwa hivyo. Yule Mtu. Kwa hiyo Yesu alisema kama . . .

Wakasema, "*Sasa* tunaamini. *Sasa* tunaamini ya kwamba Wewe unajua mambo yote wala huna haja ya mtu akufundishe. Sisi . . ."

Yesu akasema, "Je, mnasadiki sasa?" Mnaona?

Hebu tuuimbe, "Sasa naamini, Bwana. Umefanya ya kutosha, umetupa Roho Mtakatifu, ulitupa kunena kwa lugha."

249 Sasa, ni Wapentekoste wangapi walio hapa? Hebu tuone mikono yenu. Vema. Sasa, hivi Biblia haisemi, Paulo alisema, yule Paulo mashuhuri alisema, "Kama kuna . . . Kama ninyi nyote mkinena kwa lugha, na wasio na elimu waingie, na—nanyi nyote mnanena kwa lugha, watasema mna wazimu. Lakini kama mmoja akiwa ni nabii, naye atafunua siri za moyo, basi wataanguka chini, waseme, 'Kweli Mungu yu pamoja nanyi.'" Hiyo ni kweli? Pentekoste hasa inakuja. Mnaona? Mnaona? Msiondoke mwingie katika mwenendo wa ulimwengu, dumuni Pentekoste.

250 Ninyi nyote Wamethodisti humu ndani, ni wangapi humu ndani waliokuwa Wamethodisti hapo awali? Hebu tuone mikono yenu. Mnaona? Ni wangapi waliokuwa Wabaptisti? Ushikilie mkono wako. Ni wangapi waliokuwa Wapresbiteri? Ushikilie mkono wako. Wangapi walikuwa Wakatoliki? Ushikilie mkono wako. Mnaona? Imetokea nimekwambia, ewe rafiki, ninatoka kwenye familia ya Kikatoliki, pia. Mimi ni Muairishi. Hiyo ni kweli.

251 Mkatoliki, nikihojiwa na kasisi fulani hivi majuzi, si, ama, si hivi majuzi, muda mrefu uliopita, walisema, "Kama hili ni la Mungu, karama zote za kweli zinarudi kwa kanisa mama."

252 Nikasema, "Nimerudi kwenye Kanisa mama tangu nilipompokea Roho Mtakatifu." Nikasema, "Unamaanisha mama wa madhehebu, sio Kanisa mama. Tunazaliwa ndani Yake, sio kuunganishwa ndani Yake, kuzaliwa ndani Yake." Hiyo ni kweli. Vema.

Sasa naamini, (Umefanya vya kutosha, Bwana,
naamini sasa.) sasa naamini,
Mambo yote yanawezekana, (Mnaliamini?)
sasa naamini;
Sasa naamini, sasa naamini,
Mambo yote yanawezekana, sasa naamini.

253 Sasa hebu na tuubadilishe, tukisema, "Sasa napokea." Weka mkono mmoja moyoni mwako, huo mwingine umwinulie Mungu.

Sasa . . . (Kuna zeri katika Gileadi,
mnaipokea?) sasa napokea,
Mambo yote yanawezekana, sasa napokea;
Sasa napokea, sasa napokea,
Mambo yote yanawezekana, sasa napokea.

254 Sasa, je, amefanya mambo yote vizuri? Je, amefanya mambo yote aliyoahidi kufanya? Hiyo ni kweli. Sasa, hebu na tuinamishe vichwa vyetu pamoja, na sote, Yeye alisema, "Kwa njia hii, inawapasa kuomba," sote pamoja:

Baba yetu uliye Mbinguni, Jina Lako litukuzwe.
Ufalme Wako uje. Mapenzi Yako yafanyike duniani, kama huko Mbinguni.
Utupe leo riziki yetu ya kila siku.
Na utusamehe makosa yetu, kama sisi nasi tuwasamehevyo wanaotukosea.
Na usitutie majaribuni, bali utuokoe na uovu: Kwa kuwa Ufalme ni Wako, na nguvu, na utukufu, hata milele. Amina.

Unasema, "Kwa nini ukafanya hivyo, Ndugu Branham?"

255 Katika maombi . . . Yeye alisema, "Namna hii," kila kitu kimefanywa. Ulisema nini mle ndani? "Utuokoe na uovu, kutokuamini kwote, maradhi yote, magonjwa yote, mateso yote, ushirikina wote, kila kitu. Utuokoe na uovu."

256 Sasa, mnajua nisingeweza kushuka kwenye mstari huo kwa upambanuzi, Ninge—ningezimia kabisa kabla sijafika katikati yake. Sasa, kesho usiku tutakuwa na mstari wa upambanuzi mahali hapo pengine; usiku wa leo, tutawaombea watu hawa.

257 Ni wangapi wenu kwenye mstari huo sasa walio na uchaji, wanaona jinsi hiyo . . . ? Ninataka kuuliza, mnanena kuhusu mwujiza, mtu angewezaje, mwanadamu kama mimi, kuyajua mambo hayo? Nisingeweza kuyajua. Ni wangapi wenu wanaoamini ya kwamba hilo ndilo jambo lile lile ambalo Bwana wetu Yesu alifanya? Mnaamini? Vema basi, huo upako ambao nimewaambia habari zake, na kuwahubiria kweli, sasa Yesu ameshuka na kuthibitisha hilo ni kweli. Hiyo ni kweli? Ndipo, Yeye akasema, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio." Hiyo ni kweli? Sasa, hilo linanifanya mwaminio. Hiyo ni kweli? Sasa, kile Yeye alichosema kitakuwa mwaminio? "Wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya." Hiyo ni kweli?

Sasa nataka kuwaonyesha jambo fulani:

258 Wachungaji, wainjilisti, wamishenari, ni wangapi wenu ninyi nyote walio waaminio? Mnaona? Sasa, nitawaomba wote wenu ninyi nyote wawezao, waje moja kwa moja hapa pamoja nami. Mnaona?

259 Mimi—mimi . . . Sio, kumwacha mwinjilisti ashughulikie kila kitu, hao watu, sitaki mjenge imani yenu katika mwinjilisti, ninawatakeni imani yenu ijengwe katika mchungaji wenu wenyewe. Yeye ndiye mtu atakayewaongoza tangu sasa na kuendelea, mnaona. Na watu hawa . . .

Shukeni, baadhi yenu ndugu. Shukeni mje hapa, hebu na tufanye mistari miwili. Naam, mistari miwili.

260 Watu hawa ni watu wa Mungu wanaoamini. Nitasimama moja kwa moja katikati yao, na tutaomba. Ni wangapi huko nje watakuwa wakiwaombea, pia, huko nje? Inua mkono wako.

Kumbukeni, kuna mama wa mtu fulani, kuna baba wa mtu fulani, kuna kipenzi cha mtu fulani, mtoto wa mtu fulani. Hiyo ni kweli? Vema, vipi kama ilikuwa ni wewe? Vipi kama ilikuwa ni mama yako? Vipi kama ilikuwa ni mtoto wako? Vipi kama ilikuwa ni dada yako, mke wako, mume wako? Ungetaka mtu awe mwaminifu, sivyo?

Sasa, tutaomba, na watu hawa wote wa Mungu. . .

261 Njoni moja kwa moja hapa, ndugu, mkitaka. Njoni tu moja kwa moja *huku*, na mfanye mistari miwili. Mnajua nini? Nitawaambia, inanifanya nijivune moyoni mwangu na kushukuru kuwapata watumishi wa Mungu ambao watasimama mbele ya watu na kusema, “Mimi ni shahidi wa Injili hii, pia.”

262 Hivi hamjivunii wachungaji wenu? Semeni, “Bwana asifiwe,” kama mnajivunia wachungaji hawa. Tunajivunia ndugu zetu. Amina. Tunawajivunia. Wao ni wachungaji wenu. *Mchungaji* maana yake ni “mlishaji.” Hawa, kila mmoja wa watu hawa ana upako wa kuweka mikono juu ya wagonjwa kadiri nilivyo nao mimi.

263 Sasa, mimi si mhubiri, wao ni wahubiri, wana afisi ya juu kuliko niliyo nayo, yangu ni ofisi ya kinabii, kutabiri. Sasa, wao sivyo, hawakuumbwa kwa ajili ya jambo hilo, hawakukusudiwa hilo. Lakini Biblia inasema nini? “Mungu ameweka kanisani, mitume,” hao ni wamishenari, “manabii, wachungaji, waalimu, wainjilisti.” Hiyo ni kweli? Hizo ni karama, zilizochaguliwa na Mungu na kutiwa mafuta.

264 Sasa, mimi sina elimu, hiyo ndiyo sababu nasema mimi si mhubiri. Watu hawa wangeweza kuchukua Neno hili, wala isingewabidi kutumia moja ya karama hizi, wangeweza tu kuliweka Neno hilo huko nje wapate kumfunga Shetani katika fundo kubwa sana asingeweza kujifungua. Mnaona? Lakini siwezi kufanya hivyo, huo si wito wangu. Wameitiwa hilo. Sasa, lakini wao ni—wao ni watu wa Mungu, kila mtu aliyeitwa na Mungu ameagizwa kuweka mikono juu ya wagonjwa, nao watapata afya. Ni wangapi wanaoamini hilo? Basi utakosaje kupata afya, ukipitia kwenye tao kama hili?

265 Je, umewahi kuona jinsi Sulemani alivyojenga hekalu lake? Sikilizeni kwa makini, ulipoingia mlangoni, ilikuwaje? Kulikuwako na Malaika waliochongwa kwa mzeituni huku mabawa yao yameelekea upande wa pili, kwamba kila mwabuduo anayekuja kwenye kiti kitakatifu, alipitia moja kwa moja nchani mwa mabawa haya ya Malaika, moja kwa moja mpaka kwenye kiti cha rehema, moja kwa moja madhabahuni. Mnajua utaratibu wa hekalu la Sulemani.

266 Vema, *malaika* ni nini? “Mjumbe.” Chukua kamusi uone maana ya *malaika*. Baadhi yao ni wajumbe wa Kimbinguni, baadhi yao ni wajumbe wa duniani, ambao Mungu anakaa ndani yao kuleta Ujumbe Wake wa duniani. Na hawa ni wajumbe,

malaika wa Bwana, wajumbe kwako, nao wamesimama pale wameinua mikono yao, wapate kutii yale Mungu aliyosema, "Wataweka mikono juu ya wagonjwa, nao watapata afya." Haina budi kutukia, sivyo? Mnaamini hilo, kila mmoja wenu akipitia hapa?

267 Sasa, kwenye kinanda pale, *Amini Tu*. Hebu kila mtu humu ndani uinamishe kichwa chako, ndipo watu hawa wanapopitia mstarini, tutawawekea mikono kwa ajili ya uponyaji wao. Kila mtu akiomba. Kila mhudumu, waguse wanapopita.

268 Baba yetu wa Mbinguni, tunakuletea mstari huu mkuu wa watu, wao ni wagonjwa, Bwana, ninaomba ya kwamba utamponya kila mmoja wao wanapopitia hapa chini ya upako wa watumishi Wako hawa. Jalia wapitie kwenye mstari huu na kila mmoja aponywe kabisa. Katika Jina la Yesu.

[Ndugu Branham anawaombea watu kwa dakika tano, mengi ya maneno yake hayatambuliki—Mh.] . . . ? . . .

269 Sasa wakati wamesimama, wekeaneni mikono, wekeaneni mikono sasa. Sasa, huu ndio wakati wenu wa kuninii . . . Mnaniamini?

61-0218 Zeri Katika Gileadi
First Assembly Of God Of Long Beach
Long Beach, California Marekani

SWAHILI

©2025 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org